

**FONOLOJIA YA MANENO MKOPO YA
KINYORE KUTOKA KISWAHILI**

Violet Anindo

C50/89608/2016

**Tasnifu hii imetolewa kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya
mahitaji ya shahada ya uzamili katika idara ya Kiswahili chuo**

Kikuu cha Nairobi

AGOSTI 2021

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na mtu yeyote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.



13/11/2021

Sahihi.....Tarehe.....

VIOLET ANINDO

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha Nairobi.



Sahihi.....Tarehe.....

PROF. JOHN HABWE



Sahihi.....Tarehe.....

DKT. HANAH CHAGA MWALIWA

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa babangu mpendwa Douglas Ambula na mamangu Besi Pascalia.

Wanangu wapendwa Arsene Lisimba na Shirlene Natasha

Dadangu mpendwa Jane Ambiyu Ambula. Nakupenda sana.

SHUKRANI

Shukrani zangu kwa Rabuka kwa kunifikisha hapa. Safari ilikuwa ndefu lakini kwa uwezo wake nimeikamilisha kazi hii. Nawashukuru wasimamizi wangu Profesa John Habwe na Daktari Hanah Chaga Mwaliwa kwa kuniongoza, kunielekeza na kuihakiki kazi yangu. Mchango wenu na kujitolea kwenu kumenisaidia kuikamilisha kazi hii. Asante kwa kutembea nami katika safari hii ndefu.

Shukrani zangu ziwaendee wahariri wote wa idara ya Kiswahili. Asante sana kwa kujitolea kutufunza. Uelekezi wenu na mawaidha mliyoniya yalinitia moyo na kunisaidia kuikamilisha kazi hii.

Niwashukuru wanafunzi wenzangu Otieno, Mercy, Daniel, Ruth, Agnes, Dickens, Jacinta, Lucy, Anne na Chiry. Niwashukuru walionisaidia katika ukusanyaji wa data; Newton, Obunyasi, Florence, Sarah, Michelle, Flavian na Whitney.

Walimu wenzangu; Joshua na Syengo, hamkuchoka kunisaidia, kujitolea kwenu kumekuwa kwenye manufaa kwangu.

Nimshukuru mume wangu Peter Wanyama, wewe ni kielelezo chema kwangu. Umenifaa kwa dhiki na faraja, umekuwa nami tangu mwanzo na kunisaidia kwa hali na mali. Wewe ni mmoja wa watu ambao wamenisaidia kukua kiakademia. Wanangu wapendwa Arsene Lisimba na Shirlene Natasha mmekuwa pamoja nami na kuvumilia hata wakati nilipokosa kuwa nyumbani.

Wazazi wangu wapendwa Douglas Ambula na Besi Pascalia asante kwa kunikuza na kunielimisha. Hamkukosa kunipa mawaidha na kunielekeza, mmenipenda na kunisaidia. Ndugu zangu wapendwa: Elisha, Jane, Duncan, Lydia na Rose tumekuwa pamoja kwenye meli na sasa tumevuka pamoja.

IKISIRI

Huu utafiti umechanganua mifanyiko ya kifonolojia ambayo hutokea kwenye maneno mkopo ya Kinyore kutoka Kiswahili. Tofauti baina ya Kiswahili na Kinyore ni kwamba Kiswahili kina silabi funge ambazo haziko katika Kinyore. Maneno yanapokopwa hupitia michakato mbalimbali ili kuafiki muundo wa maneno ya Kinyore. Kazi ambazo zimechapishwa katika fonolojia zina uchunguzi halisi wa kifonolojia ambao maneno mkopo hupitia lakini uchunguzi wenyewe ni mchache. Utafiti wetu ulilenga kujaza hili pengo. Mtazamo wa nadharia ya fonolojia leksika umeongoza huu uchunguzi. Kulingana na mtazamo huu uundaji wa maneno huanzia kwa maumbo ya ndani. Umbo la nje hutokana na umbo la ndani ambapo mzizi au shina huambishwa. Maneno mkopo hupitia mabadiliko mbalimbali ili yakubalike katika lugha pokezi na mabadiliko haya hutokea kwenye fonimu au silabi. Utafiti huu umethibitisha kuwepo kwa maneno mkopo ya Kiswahili katika Kinyore. Mifanyiko mbalimbali kama uchopekaji, udondoshaji na ugeuzaji maumbo imeonyesha jinsi maneno yanavyopitia mabadiliko ili yakubalike katika Kinyore. Baadhi ya irabu za maneno mkopo huimarika zinapoingizwa katika Kinyore. Maneno mkopo yaliyo na silabi ya muundo K yanapokopwa huo muundo hubadilika na kuwa KI kwa sababu Kinyore hakina muundo wa silabi wa K. Baadhi ya maneno yanapokopwa huambishwa irabu au silabi. Ukopaji umesaidia kukuza Kinyore kwani msamiati wa kufidia dhana geni umepatikana. Pia umesaidia kukuza irabu, konsonanti na silabi za Kiswahili. Utafiti huu umebainisha vigezo vya kifonolojia vilivyotumika na kuchanganua taratibu za kifonolojia na kimofolojia zilizofuatwa katika ukopaji. Uwasilishaji umefanywa kupitia njia ya maelezo, michoro na majedwali. Data ya matokeo ya uchunguzi wetu inaweza kusaidia wasomi wa isimu za lugha za kiafrika.

YALIYOMO

UNGAMO	Error! Bookmark not defined.
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI	v
ORODHA YA VIFUPISHO.....	ix
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI	1
1. 1. Tatizo la utafiti	4
1. 2 Maswali ya utafiti.....	4
1. 3 Madhumuni ya utafiti	5
1. 4 Umuhimu wa utafiti	5
1. 5 Upeo na mipaka	5
1. 6 Yaliyoandikwa kuhusu mada.....	6
1. 7 Msingi wa nadharia	8
1. 8 Mbinu za utafiti	19
1. 9 Hitimisho	20
SURA YA PILI.....	21
FONOLOJIA YA KISWAHILI NA KINYORE	21
Utangulizi	21
2. 1 Fonimu za Kiswahili	21
2. 1. 1 Irabu za Kiswahili.....	21
2. 1. 2 Konsonanti za Kiswahili	23
2. 2 Fonimu za Kinyore.....	31

2. 2. 1 Konsonanti za Kinyore.....	31
2. 2. 2 Irabu za Kinyore.....	36
2. 3 Muundo wa Silabi za Kiswahili na Kinyore	39
2. 3. 1 Silabi za Kiswahili.....	39
2. 3. 2 Silabi za Kinyore	41
2. 4 Mwingiliano wa vipengee vya kifonolojia na kimofolojia vya Kiswahili na.....	42
2. 5 Hitimisho	44
SURA YA TATU	46
MIFANYIKO YA KIFONOLOJIA.....	46
Utangulizi	46
3. 1 Mifanyiko ya kifonolojia.....	46
3. 1. 1 Fonimu	46
3. 1. 1. 1 Udondoshaji	47
3. 1. 1. 2 Uchopekaji.....	48
3. 1. 1. 3 Ubadala	50
3. 1. 1. 4 Kurefuka kwa irabu	63
3.2 Hitimisho	66
SURA YA NNE.....	67
MIFANYIKO YA KIMOFOLOJIA	67
Utangulizi	67
4.1 Nomino ngeli za Kiswahili	67
4. 2 Nomino ngeli za Kinyore	71
4. 3 Mifanyiko ya kimofolojia.....	80
4. 3. 1 Uambishi	81
4. 3. 2 Unyambuaji	83

4 . 4 Hitimisho	84
SURA YA TANO	85
MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO	85
Utangulizi	85
5. 1 Muhtasari	85
5.2 Matokeo ya utafiti.....	86
5.3 Mapendekezo	87
6.0 MAREJELEO	89
VIAMBATANISHI	92

ORODHA YA VIFUPISHO

FL	Fonolojia Leksika
I	Irabu
V	vokali
K	Konsonanti
KI	Konsonanti – Irabu
KKI	Konsonanti – Konsonanti – Irabu
KNI	Konsonanti – Nusu irabu – Irabu
KKNI -	Konsonanti – Konsonanti – Nusu irabu – Irabu
KKKNI	Konsonanti – Konsonanti – Konsonanti – Nusu irabu – Irabu
\$	Mpaka wa silabi
//	Uwasilishaji wa fonimu
[]	Unukuzi wa fonetiki
>	Mwelekeo wa mabadiliko kwa maana ya ‘hutamkwa kama’ au ‘hugeuka kuwa’

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanafafanua lugha kwa kusema kwamba ni chombo cha mawasiliano baina ya watu wenye utamaduni mmoja na hutumika katika kuelezea ulimwengu wa wazungumzaji. Mathooko (2007) anakubaliana nao anaposema kwamba lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazokubaliwa katika jamii lugha fulani ya watu kwa ajili ya mawasiliano. Mawasiliano hayawezi kuwepo bila lugha kwa watu wenye utamaduni mmoja.

Maneno yanapokopwa huchukua maendelezo ya lugha pokezi. Kulingana na Iribemwangi, na Mukhwana (2011) kukopa ndiyo mbinu itumiwayo katika uundaji wa maneno mengi katika lugha nyingi duniani. Wanasema ukopaji wa maneno huenda sambamba na urekebishaji wa neno ili lifuate kanuni za kifonolojia za lugha pokezi.

Kuna ukopaji wa aina mbalimbali. Habwe, Matei na Nyonje (2010: 155) wanaeleza aina za ukopaji kuwa; ukopaji wa tafsiri ambapo lugha pokezi huchukua maneno kutoka lugha changizi na istilahi ambazo zimebuniwa katika lugha changizi huchukuliwa na kutafutiwa visawe vyake katika lugha pokezi. Utohozi ni aina ya ukopaji ambapo maneno ya lugha changizi huchukuliwa na kupewa maendelezo ya lugha inayokopa. Katika ukopaji wa moja kwa moja au sisisi lugha pokezi huyachukua maneno jinsi yalivyo katika lugha changizi na kuyatumia vivyo hivyo bila kuyafanyia mabadiliko yoyote. Katika ukopaji wa kiisimu, lugha zinapotagusana kila mojawapo inaweza kukopa vipengele vya kimofolojia na kimofosintaksia. Lugha moja inaweza kukopa sauti ambazo haikuwa nazo awali kutoka kwa lugha nyingine. Lugha pokezi huweza kukopa maneno kutoka kwa lugha changizi na maneno yaliyokopwa huweza kufuata kanuni za lugha pokezi na kisha kuchukua muundo wa maneno ya lugha pokezi. Ukopaji ni jambo la kimsingi katika uundaji wa maneno kwa sababu maneno mengi duniani huundwa kupitia njia ya ukopaji.


Habwe , Matei na Nyonje (2010) wanasema ukopaji ni hali ya lugha moja kuchukua vipengee vya lugha nyingine na kuviingiza katika mfumo wake. Wanaeleza utohozi kama mbinu ya ukopaji ambayo huchukua maneno kutoka kwa lugha changizi na kuyapa maendelezo ya lugha inayokopa. Utohozi hutumiwa kufidia tatizo la kukosekana kwa istilahi katika lugha changizi. Mulwa (2014) akiwanukuu Whitely, (1967), Lyons, (1968), Bynon, (1977), Mbaabu, (1996), na Mwita (2009) anasema maneno mkopo ni uhamishaji wa leksia zozote lakini ni nomino ndizo

hukopwa kwa wingi ili kuelezea dhana geni katika lugha pokezi. Tunaafikiana na hawa wataalamu kwa sababu Kinyore kimekopa maneno mengi ya Kiswahili ili kuelezea dhana ambazo hazikuwepo katika utamaduni wake. Wazungumzaji wa lugha mbili wanapotagusana ukopaji hutokea na msamiati ndio hukopwa zaidi ili kufidia tatizo la kukosekana kwa msamiati fulani katika lugha pokezi.

Lugha ya hadhi ya chini hukopa kutoka kwa lugha ya hadhi ya juu. Tukilinganisha Kiswahili na Kinyore Kiswahili kina hadhi ya juu kuliko Kinyore kwani Kiswahili ni lugha rasmi na ya taifa kulingana na katiba ya Kenya (2010). Ukopaji hupelekea lugha yenye hadhi ya chini kupata msamiati kutoka kwa lugha yenye hadhi ya juu wazungumzaji wa hizo lugha mbili wanapotagusana.

Kinyore hujulikana pia kama Olunyole na ni mojawapo ya lahaja kumi na saba za Kiluhya. Huzungumzwa na waluhya kutoka sehemu za Luanda na Emuhaya zinazopatikana katika gatuji la Vihiga. Kiluhya ni lugha inayopatikana magharibi mwa Kenya na huzungumzwa katika magatuji ya Kakamega, Busia, Bungoma, Vihiga na sehemu kubwa katika gatuji la Trans-nzoia. Kiluhya kina lahaja kumi na saba na baadhi ya lahaja za Kiluhya ni; Kimaragoli, Kibukusu, Kitachoni, Kimarama, Kiidakho, Kiisukha, Kinyore, Kitiriki, Kisamia, Kikisa, Kinyala, Kikhayo, Kiwanga, Kikabras, Kimarachi, Kitsotso (Were1967). Makundi yanayounda Kiluhya ni kumi na saba na yanapatikana katika sehemu tofauti za magharibi mwa Kenya.

Malanda (2005) akiwanukuu Were, (1967), Itabete, (1974), Angogo, (1983), na Oluoch, (2014), anasema kwamba Kiluhya kina lahaja kumi na saba. Itabete (1974) anaziweka hizi lahaja katika makundi manne: kaskazini, kati, mashariki na kusini. Angogo (1983) anaweka hizi lahaja katika makundi matatu: kaskazini, kati na kusini. Kiluhya kimegawika katika makundi matatu; kusini, kati na kaskakazini.



Lahaja tuliyoishughulikia ni Kinyore ambayo iko katika kundi la kati. Lahaja nyingine katika hilo kundi ni Tachoni, Wanga, Marama, Tsotso, Kisa na Kabras.

Mwaliwa (2000) anasema kwamba Kiswahili ni mojawapo ya lugha za kibantu kwa kuangazia muundo wake ulio sawa na lugha nyingine za kibantu. Anaungwa mkono na Mwaliwa (2014) akimnukuu Guthrie (1970) anaposema kwamba Kiswahili ni mojawapo ya lugha za kibantu zinazopatikana katika maeneo ya Afrika mashariki na kati. Muundo wa maneno ya Kiswahili ni sawa na muundo wa maneno kutoka lugha nyingine za kibantu.

Shidiavai (2015) akimnukuu Massamba (1990) anasema kwamba Kiswahili ni lugha ya kwanza kwa watu wa mwambao wa Afrika. Bakari (1982) anasema kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya kwanza ya kiafrika izungumzwayo na watu wengi sana katika Afrika mashariki na kati. Kiswahili ni lugha ambayo inatumiwa na wazungumzaji wengi kutoka maeneo ya Afrika mashariki na ni mojawapo ya lugha za kwanza katika sehemu hizo.

Mulwa (2014) akiwanukuu Massamba na wengine (1999:2) anasema Kiswahili kinazungumzwa na zaidi ya watu milioni sitini katika bara la Afrika katika nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Congo, Rwanda, Burundi, Mozambique, Zambia na Malawi. Anaendelea kusema kwamba Kiswahili kinazungumzwa nje ya bara la Afrika ambapo kinafunzwa katika vyuo vikuu kama Marekani na Uchina. Kiswahili kinatumika katika vituo vya kutangaza habari kama idhaa ya taifa (KBC) hapa Kenya, Redio Tanzania kule Tanzania, Sauti ya Marekani (Voice of America) na kule Uchina. Kiswahili ndiyo lugha inayotumika sana katika mawasiliano katika bara la

Afrika hasa Afrika mashariki. Kiswahili hutumika sana katika harakati za kila siku katika maeneo ya Afrika mashariki.

1. 1. Tatizo la utafiti

Maneno mkopo ya Kinyore kutoka Kiswahili yamepitia michakato mbalimbali ili kuafiki mfumo wa Kinyore. Tofauti inayobainika kati ya Kiswahili na Kinyore ni kwamba kuna tofauti baina ya konsonanti na silabi za Kiswahili na Kinyore. Kiswahili kina silabi funge ilhali Kinyore hakina. Mabadiliko ya sauti hutokea wakati maneno hukopwa kutoka Kiswahili hadi Kinyore. Maneno yanapokopwa kutoka Kiswahili hadi Kinyore mabadiliko ya kifonolojia hutokea. Ochilo (2018) akimnukuu Lehrer (1974) anasema kwamba wakati wa ukopaji vipengee vya isimu ndivyo hukopwa zaidi. Kinyore kimekopa vipengee vya kiisimu kutoka Kiswahili. Maneno yanapokopwa hupitia michakato mbalimbali ili kuafiki muundo wa maneno ya lugha pokezi ambapo hapa ni Kinyore. Mabadiliko hutokea kwenye vokali, konsantsanti na silabi wakati wa ukopaji. Wakati wa ukopaji lugha pokezi ndio huamua muundo wa maneno yanayokopwa. Mwaliwa (2014) akiwanukuu Paradis na Lacharite (1997:380) anasema kazi ambazo zimechapishwa katika fonolojia zina uchunguzi halisi wa kifonolojia ambao maneno mkopo hupitia lakini uchunguzi wenyewe ni mchache. Utafiti wetu ulijaza hili pengo kwa kuangazia michakato mbalimbali ya kifonolojia ambayo maneno mkopo ya Kinyore hupitia yanapokopwa kutoka Kiswahili. Nadharia ya fonolojia leksika ilitusaidia katika kuweka wazi michakato ambayo maneno mkopo ya Kinyore kutoka Kiswahili hupitia ili yakubalike katika Kinyore.

1. 2 Maswali ya utafiti

- 1) Fonolojia ya Kinyore na Kiswahili ni ipi?
- 2) Ni mabadiliko gani ya sauti ambayo hutokea wakati maneno ya Kiswahili hukopwa na
kuingizwa katika Kinyore?
- 3) Ni mabadiliko gani ya kimofolojia hutokea wakati maneno hukopwa kutoka
Kiswahili na kuingizwa katika Kinyore?

1.3 Madhumuni ya utafiti

- 1) Kueleza mfumo wa kifonolojia wa kinyore na Kiswahili.
- 2) Kubaini mabadiliko ya sauti yanayokumba maneno mkopo ya Kinyore kutoka Kiswahili.
- 3) Kubaini mabadiliko ya kimofolojia yanayokumba maneno mkopo ya Kinyore kutoka Kiswahili.

1.4 Umuhimu wa utafiti

Utasaidia watafiti wa baadaye watakaokuwa wanatafiti lugha za kibantu. Utatumika katika isimu linganishi hasa kwa wale watafiti watakaokuwa wakilinganisha Kiswahili na lugha za kibantu kwani unahusisha lugha mbili zenye mfumo wa kimofolojia na kifonolojia unaofanana.

Utafiti huu una umuhimu mkubwa kwani data hii itawasaidia wanafunzi wageni kurekebisha makosa ya kifonolojia wanapojifunza lugha ya Kinyore. Hawa ni wanafunzi ambao hawana asili ya Kinyore kwa hivyo data hii itawawezesha kutamka na kuandika maneno ya Kinyore ipasavyo.

Utafiti huu utasaidia katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na isimu za lugha za kiasia. Taaluma ya isimu ya lugha za kiasia itaifaidika pakubwa na utafiti huu kwani utaweka wazi vipengele vya kiisimu kama vile vya kimofonolojia katika lugha za kiasia hasa ya Kinyore.

Lugha ya Kiswahili inaweza kutafsiriwa kwa lugha ya Kinyore kwa kutumia data ya maneno mkopo. Wakalimani na watafsiri wataweza kutumia data hii katika kutafsiri maneno kutoka lugha ya Kiswahili hadi Kinyore.

1.5 Upeo na mipaka

Katika utafiti wetu, tulishughulikia maneno mkopo ya Kinyore kutoka Kiswahili. Niliangazia mabadiliko ya kifonolojia yaliyokumba vokali, konsonanti na silabi. Nilihusisha wazungumzaji wa lugha za Kinyore na Kiswahili. Ingawa Kiluhya kina lahaja nyingi, nilijikita katika lahaja moja ambayo ni kinyore. Kinyore kinazungumzwa katika nchi za Kenya na Uganda, nilijikita katika Kinyore kinachozungumzwa katika nchi ya Kenya. Nilitumia nadharia ya fonolojia leksika nikiangazia Mohanan (1982) na Kiparsky (1982) ambao walitoa mchango mkubwa sana katika kuibuka kwa nadharia hii.

Wazungumzaji wa kinyore wamepakana na wazungumzaji wa lugha nyingine kama Kisa, Logoli na Tiriki na huenda wamekopa maneno tofauti kutoka lugha hizo. Utafiti wetu ulijikita tu katika maneno mkopo kutoka lugha ya Kiswahili. Madhumuni yangu ni kuchangia katika uandishi wa sarufi ya lugha ambazo nilishughulikia.

1. 6 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Mwihaki (1998) anasema kwamba maneno mkopo ni leksia ya dhana ambayo inatokana na lugha nyingine. Hayo maneno yanapoingizwa katika lugha nyingine yanatoholewa kulingana na fonolojia ya lugha pokezi. Katika uchunguzi wake ameelezea sababu zinazopelekea ukopaji na kushughulikia vigezo vya kifonolojia vya Gikuyu. Sababu kuu anayotoa iliyopelekea Gikuyu kukopa maneno kutoka Kiingereza ni mtagusano wa wazungumzaji wa hizi lugha mbili. Teknolojia na utamaduni ni sababu zingine anazoelezea kuwa zilisababisha ukopaji. Gikuyu ni mojawapo ya lugha za kibantu na baadhi ya vigezo alivyoainisha katika kazi yake vinaingiliana na vigezo vya lugha tulizofanyia utafiti. Tumeainisha vigezo vya kifonolojia tukiangazia irabu, konsonanti na silabi. Ukopaji hutokana na kuingiliana kwa wazungumzaji wa lugha mbili au zaidi na ni kutokana na mtagusano wao ambapo maneno hukopwa.

Mwita (2009) ameshughulikia maneno mkopo ya Kiswahili kutoka Kiarabu. Kazi yake inaeleza jinsi maneno ya Kiarabu yanavyoingizwa katika Kiswahili na mabadiliko yanayofanyiwa fonimu za Kiarabu ili kutosheleza muundo wa Kiswahili. Mwita ameeleza kwamba maneno mkopo katika Kiswahili yamepanua miundo ya silabi za Kiswahili. Kiswahili na Kinyore ni lugha nasaba kwani zote ni lugha za kibantu na hivyo utafiti wake ulitufaa hasa katika kubainisha mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea maneno ya Kiswahili yanapokopwa na kuingizwa katika Kinyore.

Mwaliwa (2014) akiwanukuu Anttila (1972) na Hall-lew (2002) anasema ukopaji ni kipengele cha mabadiliko katika lugha kinachohusu mwingiliano wa zaidi ya lugha moja. Anasema ukopaji hutokea wakati ambapo wazungumzaji wa lugha mbili au zaidi hutagusana. Mulwa (2014) akimnukuu Moravesiks (1978) anatoa maelezo kwamba ukopaji wa nomino ni jambo la kawaida lugha zinapotagusana. Anaendelea kusema kwamba wazungumzaji wanapoingiliana hukopa maneno kutoka lugha wanayoingiliana nayo na hakuna lugha ambayo wazungumzaji wake wanaweza kusema kwamba wametagusana na lugha nyingine ambayo haijawahi kukopa maneno. Wazungumzaji wa Kiswahili na Kinyore wametagusana kwa muda mrefu na kupelekea

Kinyore kukopa maneno kutoka Kiswahili. Ikiwa lugha mbili au zaidi zitatagusana basi wazungumzaji hujikuta wakitumia maneno kutoka kwa lugha nyingine pamoja na yao.

Mwaliwa (2014) akimnukuu Winford (2003:29) anasema ukopaji unaweza kutokea katika mazingira ambapo kuna mtagusano kati ya wapokezi na wachangizi katika jamii ambapo kuna uwili lugha. Anasema kukopa kwingi ambako kunahusiana na mtagusano wa mbali kunatokana na hamu ya kutaka kudhihirisha vitu vipya, watu, mahali na dhana hasa sehemu mpya za maarifa na tajriba katika utamaduni kupitia kwa kukuza sayansi na teknolojia. Utamaduni wa Kinyore umepokea dhana geni ambazo zimekosa msamiati wa kuzitajia. Kinyore kimekopa kutoka Kiswahili ili kupata msamiati wa kutajia hizi dhana geni. Ili ukopaji uweze kutokea ni lazima tuwe na makundi mawili yaani wenye kutoa msamiati na wenye kuupokea huo msamiati. Ukopaji wetu umetokea katika mazingira ya uwili lugha; Kiswahili na Kinyore.

Mwaliwa (2014) akimnukuu Haugen (1950) anasema ukopaji wa kiisimu ni jambo ambalo linatokea katika kila lugha na ni mojawapo ya mambo ambayo yanakuza na kubadilisha lugha. Akiendelea kuelezea Mwaliwa (2014) anamnukuu Hall-lew (2002) kwa kusema kwamba kila wakati neno linapokopwa mara nyingi fonolojia ya lugha pokezi huathiriwa aidha sauti za konsonanti au irabu huathiriwa. Hii ni kwa sababu lugha pokezi hupata muundo mpya. Ochilo (2018) akimnukuu Hoffer (2000) anasema kwamba ukopaji wa kiisimu unahusu michakato ya kutoa vipengee kutoka lugha moja hadi nyingine na lugha changizi ndiyo hutoa vipengele na pokezi hupokea hivyo vipengele. Maneno mkopo ya Kiswahili yamepitia ukopaji wa kiisimu ambapo vipengee vya kiisimu vimekopwa kutoka Kiswahili na kuingizwa katika Kinyore. Mabadiliko yametokea kwenye fonimu na silabi. Maneno yaliyokopwa hupitia michakato ya kifonolojia na kuchukua miundo ya maneno ya lugha pokezi. Vigezo vya fonolojia ambavyo ni sauti za konsonanti na irabu huathiriwa wakati wa ukopaji.

Mwaliwa (2014) akiwanukuu Fromkin na wengine (2003:512) anasema ukopaji wa maneno kutoka lugha nyingine ni chanzo kikubwa cha msamiati. Mulwa (2014) akimnukuu Whitely (1963) anaeleza mambo mawili yanayosababisha ukopaji kuwa mahitaji na hadhi. Kwa kuangazia hadhi mtu hutaka ajitambulisha na kikundi mahususi. Lugha ambayo huchukuliwa yenye hadhi ndiyo inayokuwa changizi na lugha ambayo hutumiwa zaidi katika eneo fulani mara nyingi ndiyo hukopwa. Kiswahili kina hadhi ya juu kuliko Kinyore na kusababisha Kinyore

kukopa kutoka kwa Kiswahili. Ukopaji hukuza msamiati wa lugha pokezi na ni mahitaji ndiyo yanayofanya lugha ikope. Kinyore kimekua kwa sababu ya ukopaji.

Ochilo (2018) akimnukuu Haspelmath (2008) anasema kwamba kunaweza kuwa na tukio ambapo tayari neno lipo katika lugha pokezi lakini wazungumzaji wake hukopa neno jingine na kulifanya hilo neno likubalike katika lugha yao na liweze kutumika kama lile linalopatikana katika lugha pokezi. Hayo maneno mawili basi huwa visawe. Kinyore kimejikuta na msamiati zaidi ya mmoja wa kutajia dhana. Hii ni kwa sababu tayari dhana hiyo ilikuwa na msamiati katika Kinyore kabla ya kuukopa ndiposa kukawa na zaidi ya msamiati mmoja wa kutajia dhana.

Mwaliwa (2014) akimnukuu Hall-lew (2002) aliyemnukuu Fantiris (1985) kwa kutumia ngazi zake za ukopaji ambazo ni: ukopaji ambapo neno halipitii mabadiliko yoyote linapoingizwa katika lugha pokezi na ukopaji ambapo neno hupitia mabadiliko kabla ya kuingizwa katika lugha pokezi. Kuna baadhi ya maneno mkopo kutoka Kiswahili ambayo hayapitii mabadiliko yoyote yanapoingizwa katika Kinyore. Maneno mengine yanapokopwa na kuingizwa katika Kinyore yanapitia mabadiliko ndiposa yaweze kukubalika. Neno linapokopwa linaweza kubadilika au lisibadilike. Kuna baadhi ya maneno ambayo hupitia mabadiliko yanapokopwa na mabadiliko haya hutegemea mfumo wa sauti wa lugha pokezi.

1. 7 Msingi wa nadharia

Fonolojia leksika ni nadharia iliyojengwa katika miaka ya themanini na mawazo na utafiti wa wanaisimu mbalimbali akiwemo Kiparsky (1982-1985) na Mohanan (1982). Kiparsky (1982) anasema kwamba sheria za kifonolojia hufanya kazi sanjari na zile za kimofolojia katika leksika.

Chomsky na Halle (1968) wanasema kwamba vipande katika lugha si kitengo cha mwisho katika muundo wa kifonolojia. Wanaangazia vipande kama vilivyoundwa kwa elementi ndogo zinazoitwa sifa. Hiki ndicho kitengo cha muundo wa kifonolojia kinachounda vipande. Uwakilishi wa kipande kilicho na sifa unaweza kukamilika kwa kuweka sifa za kila kipande katika matriki. Uwakilishi huu unaeleza ya kwamba kipande kitakuwa [+] ikiwa kitakuwa na sifa na [-] ikiwa kitakosa sifa fulani. Hii kazi ni ya kimsingi katika fonolojia zalishi na itatupa data kuhusu sifa za kifonolojia zitakazotupa uelewa kuhusu mfumo wa sauti za Kinyore.

1. 7. 1 Mihimili ya nadharia ya fonolojia leksika

Mihimili muhimu iliyowekwa na waasisi wa nadharia ya fonolojia leksika ni mhimili wa ngazi leksia, mpangilio wa viambishi, kanuni ya kimzunguko na kanuni ya kufuta mabano.

i) Kanuni ya ngazi leksia.

Nadharia ya fonolojia leksika inaeleza kwamba maneno yana mpangilio fulani wa viwango. Kiparsky (1982) anasema viambishi hufanya kazi tofauti katika michakato ya uundaji wa maneno. Katika mchakato wa uundaji wa maneno viambishi vya unyambuaji na uambatanishaji vinaweza kuwekwa kwenye mfuatano wa viwango mbalimbali vilivyo na uhusiano. Kwa hivyo michakato ya kifonolojia hufanyika kwenye kiwango cha kwanza cha sehemu ya mofolojia. Kanuni za kifonolojia zinatumiwa katika kiwango hicho hicho cha kwanza. Matokeo ya kiwango cha kwanza cha mofolojia hutumia kanuni za kifonolojia cha kiwango cha kwanza. Matokeo ya kiwango cha kwanza cha fonolojia yanapelekwa kwenye sehemu ya mofolojia katika kiwango cha pili. Tunalomaanisha hapa ni kwamba kanuni za fonolojia zinatumiwa katika uundaji wa baada ya kila hatua ya kimofolojia na matokeo ya michakato ya kifonolojia husaidia katika kuendeleza mifanyiko ya kimofolojia. Kwa hivyo uundaji wa maneno huhusisha sehemu za fonolojia na mofolojia.

Hii kanuni inazingatia kwamba maumbo ya maneno huweza kuelezwa kupitia maumbo ya kisarufi. Msemaji anapounda maneno akilini mwake, huanza kwa ule mzizi wa neno kisha akaongeza viambishi awali na tamati.

Hii kanuni ya viwango inamaanisha kwamba maneno hupangwa kingazi katika viwango. Kwa hivyo maneno hupangwa kingazi katika mizizi, shina na viambishi kulingana na mpangilio wa viwango. Viambishi vya kiwango cha kwanza huwa karibu na mzizi na viambishi vya kiwango cha pili huwa kwenye sehemu ya nje.

1. Mfano:

Chez

Chez-a

na-chez-a

a-na-chez-e-sha

Kulingana na nadharia ya fonolojia leksika maneno huundwa kingazi. Wanafonolojia wamependekeza viwango tofauti kulingana na fasiri zao za maneno.

Kiparsky (1982) alipendekeza viwango vitatu ambavyo ni:

Kiwango 1 –Uambishaji na uambatanishaji msingi bila kufuata kanuni

Kiwango 2 - Unyambulishi na uambatanishaji ambao huja baadaye na hufuata kanuni au utaratibu fulani.

Kiwango 3 - Uambatanishaji wa sehemu ambazo huja baadaye.


Katamba (1989) anapendekeza viwango viwili ambavyo ni:

Kiwango 1 – Uambatanishaji

Kiwango 2 - Unyambulishi

Kulingana na Kiparsky (1982) muundo wa maneno unafaa kuwa ifuatavyo:

Kielelezo 1.1 Kanuni za ngazi leksia



ii) Kanuni ya mpangilio wa viambishi

Dhana ya viwango inaweka wazi kuwa maneno yanaundwa kutoka kwa mzizi, shina na viambishi. Kama ilivyotajwa hapo awali uambishaji ni mpangilio wa kingazi ambapo viambishi vya kiwango cha kwanza vinakaribiana na mzizi kuliko viambishi vya kiwango cha pili. Akidah (2012) akimnukuu Katamba (1989:258) anafananisha huu mchakato na kitunguu ambapo anasema mzizi ndicho kiini, kiwango cha kwanza ndio sehemu ya ndani na kiwango cha pili ni sehemu ya nje. Fonolojia ya baada ya leksika husimamia sehemu ya nje ya kitunguu.

Kielelezo 1. 2 Mpangilio wa viwango vya mofolojia

Viambishi awali		Mzizi		Viambishi tamati	
	Viambishi vya kiwango 1	Mzizi	Viambishi vya kiwango 1		
Viambishi vya kiwango 2	Viambishi vya kiwango 1	Mzizi	Viambishi vya kiwango 1	Viambishi vya kiwango 2	

2. Mfano:

chez

na-chez-a

a -na-chez-e-sha

iii) Kanuni ya kimzunguko

Kama tulivyoeleza katika kanuni ya viwango, nadharia hii inaeleza kwamba kanuni za mofolojia na fonolojia hutekeleza majukumu yake kimzunguko. Hii ni kwa sababu hizi kanuni zinatumiwa kwanza kwenye mzizi kisha zinaenda nje kwenye viambishi vilivyo karibu na mzizi kisha zinaenda kwenye viambishi vilivyo kwenye sehemu ya nje kabisa. Katika nadharia ya fonolojia leksika inafaa kanuni za kifonolojia zianze kutumiwa kwa umbo msingi hadi kwenye umbo la kileksika. Massamba (2011: 132) anaziita sheria zinazofanya kazi katika uundaji wa neno sheria za fonolojia ya leksika na zile zinazofanya kazi baada ya uundaji wa neno sheria za fonolojia baada ya leksika

Hizi kanuni zimegawika kuwili:

a) Kanuni zinazohitaji matumizi ya habari za ndani za kimofolojia za neno. Hutumiwa katika leksika kama mchakato wa uundaji wa maneno.

b) Kanuni ambazo hutumika baada ya kukamilika kwa mchakato wa uundaji wa maneno ambazo huitwa kanuni za baada ya leksika. Kutofautisha katika matumizi ya kanuni husababisha viwango vitatu vya uwakilishaji wa maneno.


a) Uwakilishi msingi ambao ni uwakilishi wa kimofolojia wa mofimu.

b) Uwakilishi wa kileksika ambao ni uwakilishi wa maneno.


c) Uwakilishi wa kifonetiki ambao ni matokeo ya kanuni zote za kifonolojia za maandishi yote.

Uwakilishi wa kanuni ya viwango vitatu.

Kielelezo 1.3 Kanuni ya viwango vitatu




Kielelezo 1.4: Matumizi ya hii kanuni katika leksika.



Matokeo ya matumizi ya kanuni ya kimzunguko ya mofolojia na fonolojia ya leksika inapatikana katika kielelezo cha Kiparsky (1982).

Kielelezo 1.5 Matumizi ya kanuni ya kimzunguko katika leksika.

Leksika



Kuna hatua za baada ya leksika ambazo hazitumiki kwenye muundo wa ndani wa neno. Baada ya kutumia kanuni zote za kileksika maneno yanaweza kuwakilishwa kisintaksia kuunda miundo

ya sentensi. Kanuni za baada ya leksika ni kanuni cheleweshwa ambazo hutumika baada ya kanuni zote za kileksika zimetumika. Kanuni za baada ya leksika si za kimzunguko.

iv) Kanuni ya kufuta mabano

Hii kanuni hutumika kuelezea michakato ya kufuta mabano wakati wa uundaji wa maneno. Akidah (2012) akimnukuu Durand (1990:175) anasema hii kanuni hufuta mabano ya ndani baada ya kila kiwango. Kiparsky (1982:140) anaeleza kanuni ya kufuta mabano kuwa hufuta mabano ya ndani baada ya kila kiwango. Katika mchakato wa uundaji wa maneno, mabano huwekwa kwa kila kiwango cha mofolojia. Mabano hayo hufutwa kabla ya kuingia kwenye kiwango kingine kinachofuata. Kwa mfano, mabano huwekwa kwa kiwango kimoja ambapo kuna uambatanishaji wa kanuni za kimofolojia. Baada ya uundaji wa neno, michakato itaelekeza kwenye kiwango cha pili ambapo itabidi yale mabano ya kiwango cha kwanza yafutwe ili neno liwepo kwa michakato zaidi ya kimofolojia.

3. Mfano:

{Ku + {ib} + a}

Baada ya kufuta mabano neno huwa;

[kuiba]

1. 7. 2 Matumizi ya mihimili ya nadharia ya fonolojia leksika katika maneno mkopo ya

Kinyore kutoka Kiswahili

Nilitumia mihimili ya nadharia ya fonolojia leksika katika kuchanganua maneno mkopo ya Kinyore kutoka Kiswahili. Mihimili tuliyojadili awali ni:

- i) Kanuni ya ngazi leksia
- ii) Kanuni ya mpangilio wa viwango

iii) Kanuni ya kimzunguko

v) Kanuni ya kufuta mabano.

i) Kanuni ya ngazi leksia

Maneno ya Kinyore yamepangwa katika viwango kingazi na michakato ya kimofolojia hufanyika katika kiwango cha kwanza na mengine katika kiwango cha pili. Nitaeleza kwa kutumia viambishi awali na tamati vya maneno ya Kinyore. /ɛ/, /i/, /ɔ/

Kiamb 2	kiamb 1	mzizi	kiamb 1	kiamb 2
		Kand		
		Kand	a	
ɔ	xu	kand	a	
ɔ	xu	kand	i	lla

kand - mzizi

kanda - kitendo cha kumwambia mwingine achanganye unga

ɔxukanda - kitendo cha kuchanganya unga

ɔxukandilla - kitendo kinachoonyesha mazoea ya kuchanganya unga.

Michakato ya kupata neno *ɔxukandilla* hutendeka katika viwango tofauti tofauti tukianza kwa kuzalisha shina *kanda* kutoka kwa mzizi {kand-} baada ya kuongeza kiambishi {-a} cha kiwango cha kwanza. Tunaambisha hilo shina kwa kuongeza viambishi vya kiwango cha kwanza na cha pili.

ii) Kanuni ya mpangilio wa viambishi

Michakato ya uzalishaji huhusisha kanuni za kimofolojia na kifonolojia. Tukitumia mfano wa *ɔxukandilla*, kanuni hizo zimepangwa ifuatavyo:

{Kand - } - kidahizo cha leksika ambacho hakijakokotolewa.

{ kand-} + {-a} - kanuni ya uambatanishaji ya kuongezea viambishi ikifuatwa na kufuta mabano.

Uambishaji tamati kwa kuongezea mofimu {-a}. Huu ni uambishaji wa kiwango cha kwanza. Umbo tokeo linakuwa *kanda*.

{ xu + {kandε} } – Uambishaji awali kwa kuongezea mofimu khu na kufuta mabano. Ubadala unatokea wakati ambapo / a / inabadilika na kuwa /ε /. Huu ni uambishi wa kiwango cha kwanza. Umbotokeo ni [xukandε].

{ ɔ+ { xukandi } +lla } – Uambishaji wa mofimu {ɔ-} na {-lla} ikifuatwa na kufuta mabano. Ubadala unatokea wakati ambapo sauti / ε / inabadilika na kuwa / i /. Huu ni uambishaji wa kiwango cha pili.

[ɔxuka : ndilla] – Uambishaji umeimarisha sauti /a / na kuwa / a: /

ɔxukandilla ni Kirai kipyua baada ya kutumia kanuni za kimofolojia na kifonolojia kwa kuambisha na kuambatanisha.

iii) Kanuni ya kimzunguko

Hizi ni kanuni zinazotumika kwenye mzizi kisha zinatumiwa kwenye viambishi vya kiwango cha kwanza na baadaye kwenye viambishi vya kiwango cha pili. Kanuni za kifonolojia huanza kutumiwa kwenye umbo msingi hadi kwenye umbo la kileksika.

Nitaeleza kwa kutumia mfano wa awali wa okhukandilla;

{ ɔ + { xu + { kand } + i } + { lla } }

Kanuni za kimofolojia na kifonolojia zitaanza kutumiwa kwenye mzizi { kand- } baadaye zitatumika kwa kuambisha mzizi na viambishi vya kiwango cha kwanza { xu- } na { - i }. Uambishaji wa kiwango cha pili utafuata kwa kutumia viambishi { ɔ - } na {-lla }. Baadaye tutakuwa na kirai ɔxukandilla.

iv) Kanuni ya kufuta mabano

Hii kanuni imetumiwa katika mchakato wa kupata kirai ɔxukandilla

{ o + { xu + { kand } + i } + lla }

Uwasilishaji wa kifonetiki utatokana na kufuta mabano katika kila kiwango.

1. 8 Mbinu za utafiti

Jumla ya maneno ya Kinyore niliyokusanya kutoka kwenye maktaba na biblia ya Kinyore ni 90. Data nyingine ya maneno 90 niliitoa nyanjani. Haya ni maneno jinsi yalivyotumika na wazungumzaji wa Kinyore kwenye mikutano, shuleni na kwenye vituo vya habari kama redio. Maneno 40 ya data niliyotoa nyanjani niliyapata kutokana na kuwahoji wazungumzaji wa Kinyore na maneno 50 nilipata kwa kusikiliza redio Anyole. Kwa ujumla data niliyotumia ilikuwa ya maneno 180 na yalitoshwa kushughulikia utafiti wetu. Ili kupata data hii nilitumia mbinu ya mahojiano. Nilieleza wahojiwa kwamba msamiati wa dhana ambazo tayari tulikuwa nazo katika utamaduni wetu haukuhusu maneno mkopo. Dhana geni zilizoingia katika utamaduni wetu na zikakosa msamiati wa kuzitajia ndizo zilizosababisha ukopaji. Baada ya wao kuelewa kisababshi cha ukopaji niliwauliza wataje baadhi ya dhana geni ambazo hapo awali hazikuwa katika Kinyore lakini zilikuwa na msamiati wa kuzitajia. Data hii ilikuwa na umuhimu mkubwa kwetu kwani ilitusaidia kubaini muundo wa maneno ya Kinyore yaliyokopwa kutoka Kiswahili.

Walionipa data walikuwa wazungumzaji wa Kinyore na Kiswahili na walio na umilisi wa lugha hizo mbili mtawalia. Wazungumzaji wa Kinyore kutoka Luanda ndio walionipa data ya maneno ya Kinyore. Nilipata data ya Kinyore kutoka kanisani, kwenye mikutano mbalimbali na vituo vya redio. Nilipata data ya Kiswahili kutoka kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Walionipa data ya Kiswahili walikuwa walimu wa Kiswahili kutoka shule za upili za Hobunaka na Ebusiratsi.

Niligawa sampuli katika makundi mawili; Kiswahili na Kinyore. Nilipata sampuli kutoka kwa wazungumzaji wawili kutoka kwenye kila kikundi. Nilitumia rekoda ya simu kurekodi wahojiwa. Wazungumzaji wa Kinyore walisoma maneno ya Kinyore nikiiweka data hiyo katika ishara za kifonetiki na wazungumzaji wa Kiswahili wakasoma maneno ya Kiswahili nikiweka data ya Kiswahili katika ishara za kifonetiki. Nilitumia watu wawili ili niwe na uhakika wa data waliyonipa. Iwapo wa kwanza angekosea basi wa pili angerekebisha makosa ya mhojiwa wa kwanza.

Lugha mbili tulizofanyia utafiti ni za kibantu kwa hivyo zina muundo wa kifonolojia unaokaribiana. Tultambua maneno mkopo ya Kinyore kwa kulinganisha muundo na maana yake na ule wa Kiswahili. Zipo dhana ambazo hazikuwepo katika utamaduni wa Wanyore wa hapo awali. Leksia zinazohusu dhana geni katika utamaduni wa Wanyore ndizo zilizotusaidia kutambua maneno mkopo.

Katika uchanganuzi wetu tulumia kanuni za nadharia ya FL. Kanuni zilizotuongoza ni ngazi leksia, mpangilio wa viambishi, kanuni ya kimzunguko na ya kufuta mabano. Kuainisha sauti kulitusaidia kutambua zile sauti zilizobadilika. Sheria na vigezo vya kifonolojia vilivyotumika viliwekwa wazi baada ya kuchunguza mabadiliko ya sauti. Kigezo chochote cha kifonolojia kilizingatiwa pamoja na uhusiano wa vigezo hivi. Kanuni za fonolojia ya Kinyore ndizo zilizoelezea uhusiano wa vigezo husika.

Maelezo, majedwali na michoro ilitumiwa kuwasilisha matokeo ya uchunguzi wetu. Maelezo yalitusaidia katika ufafanuzi wa fonimu na silabi. Ufafanuzi zaidi wa vigezo vya kifonetiki ulifanywa kwa kutumia majedwali na michoro.

1. 9 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia tatizo la utafiti, maswali na madhumuni ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, nadharia iliyotumiwa katika uchanganuzi wa data na mbinu za utafiti. Tumelezea jinsi tulivyochanganua data kwa kutumia nadharia ya FL.

SURA YA PILI

FONOLOJIA YA KISWAHILI NA KINYORE

Utangulizi

Hii sura imeshughulikia konsonanti, irabu na silabi za Kiswahili na Kinyore. Tumeshughulikia fonimu za Kiswahili na Kinyore kwa sababu ndizo tulizotumia katika uchanganuzi wa data. Ufahamu wa hizi fonimu umetuwezesha kujua vipengele vilivyohamishwa kutoka Kiswahili hadi Kinyore na vile visivyohamishwa. Pia tumeangazia idadi ya fonimu za Kiswahili na Kinyore baada ya kutaja za kila lugha husika.

2.1 Fonimu za Kiswahili

Tumeshughulikia mfumo wa sauti za Kiswahili tukitolea maelezo konsonanti, irabu na silabi za Kiswahili. Tumbaini idadi ya konsonanti, irabu na silabi za lugha ya Kiswahili na kueleza aina ya silabi za Kiswahili kwa kuangazia miundo mbalimbali ya silabi hizi. Tumeleza sifa bainifu za konsonanti na irabu za Kiswahili. Fonolojia ya lugha ya Kiswahili huweza kusomwa kwa kutumia alama za kifonetiki jinsi zinavyowakilishwa kwenye chati (IPA).

2.1.1 Irabu za Kiswahili

Mwaliwa (2014) akimnukuu Ladefoged (2000) anasema kwamba irabu hutamkwa bila kubanwa au kuzuiliwa kwa hewa katika bomba la sauti. Mwaliwa (2014) akiwanukuu Abecrombie (1967) na Ladefoged (2000) anasema vigezo vya kifonolojia ambavyo hutumiwa kuainisha irabu ni; sehemu ya ulimi, mwinuko wa ulimi na hali ya midomo. Sehemu ya ulimi huonyesha mahala pa ulimi panapohusika wakati wa kutamka irabu. Irabu hutamkiwa kwa sehemu tatu; mbele, kati na nyuma. Irabu huweza kuwa [+ nyuma], [- nyuma] au [- nyuma, - mbele] (Mwaliwa 2014). Irabu hutamkiwa mbele, kati au nyuma [- nyuma], [- nyuma, - mbele] ama [+ nyuma]. /u na /ɔ/ hutamkiwa sehemu ya nyuma ya ulimi [+ nyuma]. /i/ na /ε/ hutamkiwa sehemu ya mbele [- nyuma] na /a/ hutamkiwa kati [- nyuma, - mbele].


Kigezo cha pili ni mwinuko wa ulimi. Irabu huweza kutamkwa ulimi ukiwa chini, kati au juu. Irabu huweza kuwa na sifa [+ juu], [+ chini] au [- juu, -chini] (Mwaliwa 2014). /i/ na /u/ ni

irabu zinazotamkwa ulimi ukiwa umeinuliwa juu [+ juu]. / ε / na / ɔ / hutamkwa ulimi ukiwa nusu chini [- juu, - chini]. /a/ hutamkwa ulimi ukiwa chini [+ chini].

Kigezo cha tatu ni hali ya midomo wakati wa kutamka irabu. Irabu inapotamkwa midomo hutanda au kuviringa. Irabu ikitamkwa wakati midomo imeviringa huwa [+ mviringo]. Irabu inapotamkwa wakati midomo imetanda huwa [- mviringo] (Mwaliwa 2014). Irabu inapotamkwa midomo huviringa au kutanda. Irabu ikitamkwa midomo ikiwa imetanda huwa (-mviringo) na ikitamkwa midomo ikiwa imeviringa huwa (+ mviringo). /u/ na / ɔ / hutamkwa midomo ikiwa imeviringa [+ mviringo]. /i/, / ε / na /a/ hutamkwa wakati ambapo midomo huwa imetanda [- mviringo].

Chomsky na Halle (1968) wanasema kwamba sifa bainifu imeweza kueleweka kama sifa inayoleta tofauti baina ya fonimu moja na nyingine. Katika nadharia ya fonolojia zalishi sifa huwekwa kwenye mpangilio unaoitwa matriki. Kila sifa au kundi la sifa huelezea konsonanti au irabu fulani. Sifa hizi huwakilishwa na [+] kuonyesha ya kwamba hiyo sifa iko au [-] kuonyesha ya kwamba haiko. Matumizi ya nadharia ya fonolojia zalishi katika Fonolojia Leksika yalitufaa kwani yalitusaidia kutolea konsonanti na irabu sifa bainifu.


Kielelezo 2.1 Irabu za Kiswahili




Chini a

Vigezo vya irabu za Kiswahili vimeorodheshwa hapa chini.


/a/




/ε/




/ɔ/



/i/



/u/



2. 1. 2 Konsonanti za Kiswahili

Mwaliwa (2014) akimnukuu Ladefoged (2000) anasema kwamba konsonanti hutamkwa wakati ambapo kuna msongo wa haraka wa mishipa katika mkondohewa katika bomba la sauti. Habwe na Karanja (2004:28) wanaeleza konsonanti kama sauti ya lugha ambayo hutamkwa wakati hewa ambayo hutoka mapafuni huzuiliwa kabisa au kidogo na kufanya nafasi ya hewa kuwa ndogo sana ambapo hewa hupita kwa mkwaruzo. Mwaliwa akiwanukuu Abecrombie (1967) na Ladefoged (2000) anasema kwamba wakati wa kuainisha konsonanti vigezo vinne hutumiwa navyo ni mahali pa kutamkia; namna ya kutamkwa, hali ya glota na mkondo wa hewa. Mwaliwa (2014) akimnukuu Katamba (1989) anasema kwamba mabadiliko katika mkondohewa sauti

inapotolewa huonyeshwa katika bomba la sauti na sifa za kinywani. Sifa zenyewe ni [+ au – korona], [+ au – anteria], [+ au – midomo], [+ au – nazali] au [+ au – tandaza].

Mwaliwa (2014) anasema mahala pa kutamkia huhusu ala ambazo hutatiza hewa katika bomba la sauti. Hapa ndipo hewa hubanwa kabisa au kwa kiasi na kuizuia kupita kabla ya kuachiliwa. Kwa kuangazia kigezo cha mahala pa kutamkia hewa huwa imefungiwa kabisa au kwa kiasi na ala za sauti. Uainishaji wa konsonanti kwa kuangazia mahala pa kutamkia unahusu sauti za midomo, sauti za mdomo na meno, sauti za meno, sauti za ufizi, sauti za kaaka gumu, sauti za kaaka laini, sauti za kilimi, sauti za koromeo na sauti za kongomeo ambazo pia huitwa sauti za glota (IPA 2018).

Hali ya glota ni kigezo cha koromeo ambacho huonyesha jinsi hewa huzuiliwa inapotokea mapafuni. Sauti inaweza kutamkwa kanda za sauti zikiwa zimetulia au zinasepetuka. Sauti zinazotolewa kanda za sauti zikisepetuka zinaitwa sauti ghuna na sauti zinazotolewa kanda za sauti zikiwa zimetulia ni sauti ambazo si ghuna (Mwaliwa 2014). Tukiangazia kigezo cha hali ya glota sauti itakuwa ghuna ikiwa itatamkwa kanda za sauti zikiwa zinasepetuka na si ghuna itatamkwa kanda za sauti zikiwa tuli. Sauti itakuwa ghuna au si ghuna kulingana na namna hewa inayotoka mapafuni itazuiliwa.

2.1. 2. 1 Vipasuo

Mwaliwa (2014) akimnukuu Ladefoged (2000) anasema kwamba vipasuo hutamkwa kwa kufungiwa kabisa kwa hewa na kisha kuachiliwa kwa ghafla. Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa hewa inapofungiwa hujaa nyuma ya ala inayoizuia na hiyo ala inapotolewa hewa huweza kupita kwa mlipuko. Konsonanti itaitwa kipasuo ikiwa hewa itazuiliwa kabisa na ala na kisha kuachiliwa ipite na inapopita huweza kutoa sauti kwa nguvu. Vipasuo vya Kiswahili ni /k/, /g/, /t/, /d/, /p/, /b/ na /ʃ/. Tutaangazia sifa za vipasuo vya Kiswahili.

/p/

-silabi
+anteria
-korona
-ghuna
-nasali

/b/

-silabi
+anteria
-korona
+ ghuna
-nasali

/t/

-silabi
+anteria
+ korona
-ghuna
-nasali

/d/

-silabi
+anteria
+ korona
+ ghuna
-nasali

/ʒ/

-silabi
-anteria
+ korona
+ghuna
-nasali

/k/

-silabi
-anteria
-korona
-ghuna
-nasali


/g/

-silabi
-anteria
-korona
+ghuna
-nasali


2. 1. 2. 2 Vikwaruzo

Mwaliwa (2014) akimnukuu Ladefoged (2000) anasema kwamba vikwaruzo hutamkwa wakati ambapo hewa huwa imezuiliwa kwa kiasi na sio kufungiwa kabisa. Wakati wa utamkaji wa vikwaruzo hewa huzuiliwa kwa kiwango fulani na ala za sauti. Vikwaruzo vya Kiswahili ni /v/, /f/, /z/, /s/, /h/, /ʃ/, /θ/, /ð/ na /ɣ/. Sifa za vikwaruzo vya Kiswahili ni kama ifuatavyo.


/f/




/v/




/s/




/z/




/ʃ/




/h/




/ ð /



/ θ /




/ ɣ /



2. 1. 2. 3 Vipasuo- kwaruzo

Mwaliwa (2014) akimnukuu Ladefoged (2000) anasema kwamba vipasuo-vikwaruzo hutamkwa wakati ambapo hewa hufungiwa kabisa na kisha kuachiliwa polepole. Habwe na Karanja (2004:34) wanasema kwamba wakati wa kutamka vipasuo- kwaruzo, ala za sauti hufungia hewa kabisa na kisha kuiachilia kwa ghafla ipite. Wanasema kwamba hizo ala huwa haziachani kabisa kwani mwanya mdogo huachwa ili hewa iendelee kupita. Hewa yenyewe hupita kwa shida na kusababisha mkwaruzo. Wakati wa kutamka vipasuo- kwaruzo hewa hufungiwa kabisa na ala za sauti kisha kuachiliwa kupita polepole. Kipasuo-kwaruzo cha Kiswahili ni /tʃ/. Sifa za hiki Kipasuo- kwaruzo zimeorodheshwa hapa chini.

/ tʃ /



2. 1. 2. 4 Nasali

Mwaliwa (2014) akimnukuu Ladefoged (2000) anasema kwamba nasali hutamkwa hewa ikipita kinywani na puani. Nasali si endelevi kwa sababu wakati wa kuzitamka hewa hufungwa kabisa kabla ya kuachiliwa kighafla katika bomba la sauti (Mwaliwa 2014). Nasali hutamkwa hewa inaparuhusiwa kupita puani na kufungwa kabisa isipite kinywani. Nasali za Kiswahili ni nne na ni /n/, /m/, /ŋ/ na /ɲ/ na zinapatikana katika maneno kama [mke] na [ncha]. Sifa za nasali za Kiswahili ni:

/m/

+ silabi
+anterior
-korona
+ ghuna
+ nasali

/n/

+ silabi
+anterior
+ korona
+ ghuna
+ nasali

/ɲ/

+ silabi
-anterior
+ korona
+ ghuna
+ nasali

/ŋ/

+ silabi
-anterior
- korona
+ ghuna
+ nasali

2. 1. 2. 5 Likwidi

Ni sauti ambazo wakati wa kutamkwa hewa huwa imetatizwa kwa namna maalum kwa sababu ala za sauti huwa zimekaribiana (Habwe na Karanja 2004:35). Wakati wa utamkaji wa likwidi hewa huzuiliwa kwa kiasi kisha kuachiliwa ipite kando ya ulimi (Mwaliwa 2014). Likwidi hutamkwa hewa ikiruhusiwa kupita kando ya ulimi kwa sababu huwa imezuiliwa na ala ya sauti. Tuna likwidi mbili katika Kiswahili nazo ni kitambaza /l/ na kimadende /r/. Sifa za hizi likwidi ni:

/r/	/l/
-silabi	- silabi
+anteria	+anteria
+ korona	+ korona
+ ghuna	+ ghuna
-nasali	- nasali

2. 1. 2. 6 Nusu- irabu

Mwaliwa (2014) akiwanukuu Abecrombie (2967) na Ladefoged (2000) anasema wakati wa kutamka nusu- irabu ala za sauti huwa hazijakaribiana kwa hivyo hewa haifungiwi popote ,hakuna msugano wa ala za sauti au mgusano wa ulimi na midomo. Kifonetiki, nusu- irabu zinafanana na irabu kwa sababu zinatamkwa bila kuzuiliwa kwa hewa (Mwaliwa 2014). Nusu- irabu inapotamkwa hewa huruhusiwa kupita kinywani bila kuzuiliwa na ala za sauti. Nusu- irabu za Kiswahili ni mbili nazo ni ; /w/ na /j/. Sifa za hizi nusu- irabu zimeorodheshwa hapa chini.

/w/

-silabi
 +anteria
 +korona
 +ghuna
 -nasali

/j/

-silabi
 -anteria
 -korona
 +ghuna
 -nasali

Kielelezo 2.2 KONSONANTI ZA KISWAHILI

	Midomo	Mdomo- meno	Meno	Ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaa laini	Kilimi	Koo	Glota
Vipasuo	p b			t d	ʃ	k g			
Nasali	m			n	ɲ	ŋ			
Vikwaruzo		f v	θ ð	s z	ʃ	y			h
Vipasuo- kwaruzo					tʃ				
Kitambaza				l					
Kimadende				r					

Nusu- irabu	w				j				
----------------	---	--	--	--	---	--	--	--	--

*Imetolewa kwenye chati ya IPA iliyofanyiwa marekebisho (2018)

2. 2 Fonimu za Kinyore

Kinyore kina sauti za irabu na konsonanti. Baadhi ya hizi sauti zinafanana na sauti za Kiswahili lakini tofauti inayobainika kwa baadhi inatokana na mwinuko wa ulimi, urefu wa irabu na mahala pa kutamkiwa kwa konsonanti.

2. 2. 1 Konsonanti za Kinyore

Malanda (2005) anasema kwamba konsonanti za Kinyore ni kumi na tisa na tatu kati yazo ni vipasuo, nne ni nasali, tano ni vikwaruzo, mbili ni vipasuo- kwaruzo, tatu ni likwidi, mbili ni nusu- irabu na konsonanti zilizonasalishwa ni nne. Konsonanti zenyewe alizotaja ni /β/, /p/, /f/, /t/, /s/, /h/, /tʃ/, /x/, /k/, /ʃ/, /dʒ/, /r/, /w/, /j/, /m/, /n/, /ŋ/, /ɲ/. Kinyore kina konsonanti kumi na sita kwa sababu hakina sauti ya glota /h/, /ʃ/na /dʒ/.

2. 2. 1. 1 Vipasuo

Vipasuo vya Kinyore ni / p/, / t/ na / k/. Sifa za vipasuo vya Kinyore ni;


/ p/	/ t/	/ k/
-silabi	-silabi	-silabi
+anterior	+anterior	-anterior
-korona	+korona	-korona
-ghuna	-ghuna	- ghuna
-nasali	- nasali	- nasali

Kutokana na sifa tulizotaja hapo za vipasuo vya Kinyore tunatambua kwamba vipasuo vyote vya Kinyore vina sifa zinazofana.


2. 2. 1. 2 Vikwaruzo

Vikwaruzo vya Kinyore ni / β /, / f/, / s/ na / x/ . /β/ ni kikwaruzo kinachotamkiwa midomoni. / x/ ni kikwaruzo kinachotamkiwa kwenye kaaka laini, si sauti ghuna. Sifa za vikwaruzo vya Kinyore zimeorodheshwa hapa chini.


/β/




/ f/



/ s/




/ x/



2. 2. 1. 3 Vipasuo-kwaruzo

Kinyore kina kipasuo-kwaruzo / tʃ / (Malanda 2005) . Kipasuo hiki hutamkiwa kwenye kaaka gumu na si sauti ghuna. Hapa chini ni sifa za kipasuo- kwaruzo cha Kinyore.

/ tʃ /




2.2.1.4 Nasali

Kinyore kina nasali nne anbazoni / m/, / n/, / ɲ / na / ŋ / (Malanda 2005). Lugha zote mbili zina idadi sawa ya nasali. Nasali zote za Kinyore ni sauti ghuna. Sifa za nasali za Kinyore ni sawa na za nasali za Kiswahili (tazama 2.1.2.4)


2. 2. 1. 5 Likwidi

Malanda (2005) anasema kwamba Kinyore kina likwidi mbili; kitambaza / l/ na kimadende / r/. Likwidi za Kinyore zina sifa zifuatazo.

/ l /



/ r /



2. 2. 1. 6 Nusu irabu

Kinyore kina nusu-irabu mbili ambazo ni / w / na / j / (Malanda 2005). Nusu irabu za Kinyore na Kiswahili zina sifa zinazofanana (Tazama 2. 1. 2. 6).

Konsonanti za Kinyore zimewakilishwa kiothografia na kifonetiki kama zinavyoonyeshwa katika maneno ya Kinyore hapa chini.

Kielelezo 2.3 Konsonanti za Kinyore

Othografia	Ishara za kifonetiki	Uwakilishi wa kifonetiki	Ufafanuzi
b	/β/	aβε:xɔ	ukoo
p	/p/	papa	baba
f	/f/	ɔlufu/	kifo
t	/t/	litu:ma	hindi
s	/s/	ɛsiεɔ	ufagio
ch	/tʃ/	ɛtʃai	chai
kh	/x/	/lixɔβa/	ngozi
k	/k/	/ɔmukunda/	shamba

l	/l/	lilɔβa	mchanga
r	/r/	ɔmurwε/	kichwa
w	/w/	ɔlwana	utoto
y	/j/	lijai	yai
m	/m/	mama	mama
n	/n/	ɛlino	jino
ng'	/ŋ/	liŋa:ŋa	ndege
ny	/ɲ/	ijumba	nyumba

*Baadhi nimetoa kwa Malanda (2005).

Kielelezo 2.4 konsonanti za kinyore

	Midom o	Mdomo- meno	Meno	Ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaa laini	Kilimi	Koo	Glota
Vipasuo	p			t		k			
Nasali	m			n	ɲ	ŋ			
Vikwaruzo	β	f		s		x			

Vipasuo-kwaruzo					tʃ				
kimadende				r					
Kitambaza				l					
Nusu-irabu	w				j				

2. 2. 2 Irabu za Kinyore

Kinyore kina irabu kumi ambapo tano ni fupi na tano ni ndefu na irabu zenyewe ni / i/, / I/, / u/, / u /, / e/, / ε /, / o/, / o /, / a/ na / ɜ / (Malanda 2005). Ochilo (2018:25) hakubaliani na Malanda anaposema Kinyore kina irabu tano ambazo ni / I/, / u /, / ε /, / o / na / a/ na kuweka Kinyore katika kundi la lugha za kibantu zilizo na irabu tano (Guthrie 1948: 45). Kinyore kina irabu kumi ambapo tano ni fupi na tano ni ndefu. Irabu za Kinyore ni / i/, / i:/, / u/, / u:/, / ε /, / ε :/, / o /, / o :/, / a/ na / a:/ . Sifa za irabu za Kinyore ni:

/ a/	/ ε /	/ i/
$\left(\begin{array}{l} + \text{silabi} \\ - \text{ndefu} \\ - \text{nyuma} \\ - \text{mviringo} \\ + \text{chini} \end{array} \right)$	$\left(\begin{array}{l} + \text{silabi} \\ - \text{ndefu} \\ - \text{nyuma} \\ - \text{mviringo} \\ - \text{juu} \\ - \text{chini} \end{array} \right)$	$\left(\begin{array}{l} + \text{silabi} \\ - \text{ndefu} \\ - \text{nyuma} \\ - \text{mviringo} \\ + \text{juu} \end{array} \right)$

/ a: /

(+ silabi
+ ndefu
-nyuma
-mviringo
+ chini)

/ ε: /

(+ silabi
+ ndefu
- nyuma
- mviringo
- juu
- chini)

/ i: /

(+ silabi
+ ndefu
- nyuma
- mviringo
+ juu)


/ ɔ /

(+silabi
-ndefu
+ nyuma
+ mviringo
-juu
-chini)


/u/

(+ silabi
- ndefu
+ nyuma
+ mviringo
+ juu)


/ɔ:/



/u:/



Kielelezo 2.5 Irabu za Kinyore



2. 3 Muundo wa Silabi za Kiswahili na Kinyore

Mulwa (2014) akimnukuu Goldsmith (1990: 153) anasema kwamba silabi inapatikana katika uwakilishi wa kimofolojia. Shidiavai, M . S (2015) akimnukuu Roach (2000:70) anaeleza sehemu za silabi kuwa tatu : kilele au kiini (nucleus), mwanzo au kitangulizi (onset) na koda au mwisho (coda). Anaungwa mkono na Mgullu (1999:73). Kilele mara nyingi huwa nazali au irabu ambayo hujisimamia kama silabi. Habwe na Karanja (2004) wakimnukuu Wehmeier (2000) wanasema kwamba silabi inaweza kuwa konsonanti, vokali pekee, konsonanti moja au zaidi zikifuatwa na vokali. Silabi ni kipashio kinachohusika katika uundaji wa maneno na huwakilishwa kama irabu, konsonanti na irabu au zaidi ya konsonanti moja na irabu.

2. 3. 1 Silabi za Kiswahili

Kamusi ya isimu na lugha (TUKI, 1990) inaeleza silabi kuwa kipashio cha utamkaji kilicho kikubwa kuliko fonimu na kidogo kwa neno. Silabi funge na silabi wazi ni aina mbili ya silabi za Kiswahili. Silabi wazi ni zile ambazo hazina konsonanti ambayo inafuata kilele (mwisho au koda) na huishia kwa irabu kwa mfano ta \$ ma \$ ti. Silabi funge huishia kwa konsonanti. Maneno mengi yasiyo na asili ya kibantu ndiyo huwa na silabi funge.

2. 3. 1. 1 Miundo ya silabi za Kiswahili

Kiswahili sanifu kina miundo mbalimbali ya silabi.

i) Muundo wa Konsonanti na Irabu (KI)

Huu ndio muundo unaopendelewa sana ulimwenguni katika lugha zote (Mgullu 1999:73). Miundo tofauti tofauti ya silabi huweza kuwasilishwa kutokana na muundo huu.

4. Mifano:

ga\$ri

pa\$ka

ii) Muundo wa Konsonanti (K)

Ni muundo ambapo konsonanti huwa silabi na hizi konsonanti huwa nasali mbili ambazo ni |n| na |m|.

5. Mfano:

m\$ku\$li\$ma

iii) Muundo wa Irabu (I)

Silabi ya huu muundo huwa irabu pekee.

6. Mifano:

o\$a

u\$nga

po\$a

iv) Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Irabu (KKI)

Huu muundo huwa na konsonanti mbili zikifuatwa na irabu.

7. Mfano :

Ji\$fy\$a

v) Muundo wa Konsonanti, Konsonanti, Konsonanti Irabu (KKKI)

Muundo huu unahusu konsonanti tatu zikifuatwa na irabu.

8. Mfano:

Mbwe\$ha

vi) Silabi Funge

Ni muundo ambao mara nyingi hupatikana katika maneno yaliyokopwa. Konsonanti hupatikana mwishoni mwa hizi silabi.

9. Mifano:

mak\$ta\$ba

daf\$ta\$ri

ma**sa**\$l\$he\$ri

2.3.2 Silabi za Kinyore

Kinyore ni lahaja iliyo na silabi zenye miundo tofauti ambayo hukaribiana sana na miundo ya silabi za Kiswahili sanifu. Miundo ya Kinyore ni konsonanti na irabu (KI), na irabu(I)

i) Muundo wa Konsonanti na Irabu (KI)

Maneno mengi ya Kinyore yana huu muundo kama ilivyo katika Kiswahili.

10. Mifano:

Si\$na (cheza)

te\$kha (pika)

ba\$kha (paka)

ii) Muundo wa Irabu (I)

Muundo huu unafanana na ule wa Kiswahili.

11. Mifano:

a\$ba\$a\$na (watoto)

li\$ya\$si (yai)

i\$nji\$la (ingia)

2. 4 Mwingiliano wa vipengee vya kifonolojia na kimofolojia vya Kiswahili na Kinyore

Japo vipengele vya kifonolojia na kimofolojia vya Kiswahili na Kinyore vinafanana na kutofautiana, vinafungamana kwa kiasi kikubwa sana. Lugha hizi mbili zinawiana katika vipengele vya kifonolojia na kimofolojia. Ili kupata tofauti na kufanana kwa hizi lugha mbili tulizilinganisha katika hii sehemu.

2. 4. 1 konsonanti

Kiswahili kina konsonanti ishirini na tano ambazo ni /p/, /t/, /d/, /J/, /k/, /g/, /m/, /n/, /ɲ/, /f/, /v/, /θ/, /ð/, /s/, /z/, /ʃ/, /ʒ/, /ʎ/, /ʝ/, /tʃ/, /h/, /l/, /r/, /w/, /j/. Konsonanti za Kinyore ni kumi na sita nazo ni /p/, /f/, /t/, /s/, /β/, /x/, /k/, /l/, /tʃ/, /r/, /w/, /j/, /m/, /n/, /ɲ/, /ŋ/.

Vipasuo vya Kiswahili ni saba navyo ni /p/, /b/, /t/, /d/, /k/, /g/ na /J/ na vya Kinyore ni vitatu /p/, /t/ na /k/. Sauti /b/, /g/, /d/ na /J/ ni sauti za Kiswahili na si za Kinyore. Sauti zinazopatikana katika mifumo ya lugha zote mbili ni /p/, /t/ na /k/.

Vikwaruzo vya Kiswahili ni /h/, /s/, /z/, /ʃ/, /v/, /f/, /ʎ/, /θ/ na /ð/ na vya Kinyore ni /β/, /f/, /s/ na /x/. Sauti zilizo katika Kiswahili na Kinyore ni /f/, na /s/, sauti za Kiswahili ambazo si za Kinyore ni saba /h/, /ʃ/, /ʎ/, /θ/, /ð/, /v/ na /z/. Sauti za Kinyore ambazo si za Kiswahili ni mbili /β/ na /x/. Kiswahili na Kinyore zina kipasuo kwaruzo kimoja /tʃ/.

Nasali za Kinyore na Kiswahili ni sawa kiidadi na zinafanana nazo ni /m/, /n/, /ɲ/ na /ŋ/. Maneno mkopo mengi yaliyo na hizi sauti hayapitii mabadiliko kwani nasali zilizo katika Kiswahili ndizo zilizo katika Kinyore. Lugha zote mbili tulizofanyia utafiti zina likwidi mbili ambazo zinafanana nazo ni kitambaza /l/ na kimadende /r/.

2. 4. 2 Irabu

Tulivyotaja hapo awali Kiswahili kina irabu tano na Kinyore kina kumi. Irabu za lugha zote mbili zinafungamana kwa kiasi kikubwa. Irabu za Kiswahili ni /a/, /ε/, /i/, /ɔ/ na /u/ na za Kinyore ni /a/, /a:/, / ε/, / ε:/, /i/, /i:/, / ɔ/, / ɔ:/, /u/ na /u:/.

Irabu inapotokea mahali pamoja zaidi ya mara moja tunasema kuwa hiyo ni irabu ndefu. Kinyore kilidhihirisha kuwepo kwa irabu ndefu na fupi. Fonimu kamili iliweza kuwakilishwa kwa irabu ndefu katika Kinyore. Tofauti ya maana huweza kujitokeza tunapotumia irabu ndefu na fupi

12. Mifano katika Kinyore:

Othografia	Uwakilishi wa kifonetiki	Kinyore	Tafsiri
a) /a/	/a/	/saba/	omba
b) /aa/	/a:/	/sa:ba/	osha
c) /e/	/ ε/	/amabele/	wimbi
d) /ee/	/ ε:/	/amabe:le/	maziwa
e) /i/	/i/	/sija/	udhi
f) /ii/ mchangani	/i:/	/si:ja/	toa viazi
g) /u/	/u/	/ruma/	tuma
h) /uu/ wanyama.	/u:/	/ru:ma/	kujamiana kwa

2. 4. 3 Silabi

Muundo wa silabi za Kiswahili huwa ni wa kuisha kwa irabu isipokuwa yale maneno yaliyokopwa na kuingizwa katika Kiswahili. Kinyore kina aina mbili ya miundo ya silabi yaani

konsonanti na irabu (KI) na irabu pekee(I). Kiswahili kina miundo tuliyotaja katika Kinyore na kuongezea ina muundo wa konsonanti pekee. Muundo wa konsonanti na irabu huweza kupatikana katika lugha zote mbili. Huu ni muundo ambao hutumika sana katika maneno ya Kiswahili na Kinyore na huweza kupatikana mwishoni, kati au hata mwanzoni mwa neno.

13. Mifano:

Kiswahili	Kinyore	Tafsiri
/ru\$ka/	/bu\$ku\$la/	chukua

Muundo wa silabi wa irabu pekee hujitokeza katika maneno ya Kiswahili na Kinyore. Hizi irabu huweza kupatikana katika sehemu yoyote ya neno. Irabu inaweza kupatikana katikati, mwanzoni au mwishoni.

14. Mifano:

Kiswahili	Kinyore	Tafsiri
/ju\$a/	/bo\$a/	funga
/o\$a/	/li\$a/	kula
/a\$nga/	/a\$khwe/	akupe

2.5 Hitimisho

Katika hii sura tulishughulikia mfumo wa sauti za Kiswahili na Kinyore. Tuliangazia miundo ya irabu , konsonanti na silabi . Tuliweza kuelewa jinsi Kiswahili na Kinyore zinafanana na kutofautiana . Tofauti kuu iliyobainika katika irabu ni kuwa Kiswahili kina irabu tano Kinyore kina irabu kumi ambapo tano ni ndefu na tano ni fupi. Kuna tofauti baina ya konsonanti za Kinyore na Kiswahili. Hili lilitusaidia kubaini tofauti baina ya hizi lugha mbili jambo ambalo lilitusaidia kupata muundo wa maneno mkopo ya Kinyore kutoka Kiswahili. Kiswahili na Kinyore zinafanana kwa sababu ya muundo wa silabi wa konsonanti irabu (K I) unaopatikana katika lugha zote mbili na tunafahamu kuwa huu ndio muundo unaopendelewa sana katika lugha

nyingi duniani. Miundo ya silabi ya Kiswahili ambayo haipatikani katika Kinyore itatusaidia kuleta tofauti baina ya Kiswahili na Kinyore.

SURA YA TATU

MIFANYIKO YA KIFONOLOJIA

Utangulizi

Katika hii sura tumeangazia mabadiliko tofauti ya kifonolojia ambayo maneno mkopo ya Kinyore kutoka Kiswahili hupitia ili yakubalike katika Kinyore. Tofauti kubwa baina ya hizi lugha mbili inapatikana kwenye muundo wa silabi kwani zinatofautiana kwa sababu baadhi ya silabi za Kiswahili ni tofauti na zile za Kinyore. Lugha zote mbili zinafanana kwa sababu ya muundo wa silabi ambao ni Konsonanti Irabu (KI).

3. 1 Mifanyiko ya kifonolojia

Mifanyiko ya kifonolojia huzikumba vokali na konsonanti na hutokea katika lugha nyingi za duniani (Habwe na Karanja 2004:54). Ni mabadiliko yanayotokea wakati fonimu tofauti tofauti zinapowekwa pamoja ili vipashio vikubwa kuliko fonimu viweze kuundwa. Haya mabadiliko yanaweza kuwa ya kimazingira au kimuktadha (Mgullu (1999:81).

Mabadiliko ambayo tumeangazia ni yale yanayotokea kwenye fonimu hasa konsonanti na irabu. Tumeleza michakato mbalimbali ambayo maneno mkopo hupitia ili yakubalike katika Kinyore. Tumbaini sheria mbalimbali za mifanyiko tuliyoshughulikia. Tumeongozwa na nadharia ya fonolojia leksika katika uchanganuzi wetu. Kanuni ya kimzunguko na ya ngazi leksia imetuelekeza katika utafiti huu. Kanuni ya kimzunguko imetusaidia sana hasa tulikapokuwa tukishughulikia uchopekaji na udondoshaji. Tulitumia kanuni zinazohitaji matumizi ya habari za ndani za kimofolojia ambazo hutumika kileksika kama mchakato wa uundaji wa maneno. Maneno yamepangwa kingazi kutoka kwa neno mkopo hadi linapoambishwa na kukubalika katika Kinyore. Baadhi ya maneno yameongezwa viambishi ambacho ni kitengo cha nje. Hii kanuni pia hutusaidia wakati tunakapokumbana na mifanyiko ya kimofolojia na ya kifonolojia ikitokea kwa wakati mmoja kwa mfano uchopekaji na uambishaji.

3. 1. 1 Fonimu

Katika sehemu hii tumeangazia mabadiliko ambayo hutokea kwenye irabu na konsonanti za maneno mkopo ya Kinyore kutoka Kiswahili.

3. 1. 1. 1 Udondoshaji

Huu ni mfanyiko unaoweza kutokea kwenye vitenzi, vivumishi, viwakilishi na nomino na sababu kuu ya kudondosha fonimu ni kusahilisha mawasiliano (Mgullu 1999:90).


i) Udondoshaji wa konsonanti /h/

Sauti nyingine ambazo ziko katika Kiswahili hazipatikani katika Kinyore. Maneno yanapokopwa kutoka Kiswahili na kuingizwa katika Kinyore inabidi hizo konsonanti zidondoshwe ndiposa hayo maneno yaweze kukubalika katika Kinyore.

15. Mifano:

Kiswahili sanifu	Udondoshaji na Uwakilishi wa kifonetiki	kategoria
/sahani/	/ɛsa:ni/	nomino
/cherehani/	/ɛtʃɛɾɛani/	nomino
/hoho/	/ɛɔ:/	nomino
/harambee/	/arambɛ:/	kivumishi
/ruhusa/	/ɛrusa/	kivumishi
/haleluya/	/alɛluja/	kivumishi

Sauti ya konsonanti /h/ hudondoshwa katika mazingira ya kufuatwa na irabu . Udondoshaji wa konsonanti /h/ katika maneno mkopo hutokea kabla ya irabu.



Huu udondoshaji wa konsonanti /h/ hutokea katika maneno mkopo ya Kinyore kwa sababu mfumo wa sauti ya Kinyore hauna sauti /h/ . Pili, ni rahisi kutamka silabi ya irabu pekee kuliko kutamka sauti /h/ iliyo na irabu. Tatu, inatokana na kujumlisha kwingi kwa sheria ambazo ni za lugha inayolengwa katika lugha ya kati (Selinker 1974).

3. 1. 1. 2 Uchopekaji

Ni mfanyiko unaohusu kuchopeka sauti katika maneno mkopo. Uchopekaji hutokea ili maneno mkopo yaweze kuchukua muundo wa maneno ya Kinyore na hivyo kukubaliwa katika Kinyore.

i) Uchopekaji wa konsonanti

Sauti ya konsonanti huingizwa katika maneno mkopo.

16. Mifano:

Kiswahili sanifu	Uchopekaji na Uwakilishi wa kifonetiki	Kategoria
/ɨguɔ/	/ɨnguβɔ/	nomino
/taa/	/ɛtaja/	nomino
/mbɔlea/	/imbɔlela/	nomino
/uteɔ/	/ɔlutɛlu/	nomino

Mfumo wa sauti wa Kinyore una muundo wa silabi wa Konsonanti Irabu (KI). Ili maneno mkopo yapate huu muundo konsonanti huchopekwa katikati mwa irabu mbili. Mfanyiko huu hutokea katika mazingira ya kufuatana kwa irabu mbili. Konsonanti zinazochopekwa ni zile zinazopatikana katika mfumo wa sauti ya Kinyore lakini hazipatikani katika Kiswahili. Uchopekaji huu hutokea ili kuafiki mfumo wa sauti ya Kinyore.

ii)Uchopekaji wa irabu

Kazi niliyokusanya ilikuwa na mifano ya sauti ya irabu mbili zilizochopekwa. Hizi irabu ni /u/ na /i/.

Uchopekaji wa irabu /i/

17. Mifano:

Kiswahili sanifu	uchopekaji na uwakilishi wa kifonetiki	kategoria
/mstari/	/ɔmusitari/	nomino
/ftaki/	/ɔxusitaka/	kitenzi

Uchopekaji wa irabu /u/

18. Mifano:

Kiswahili sanifu	uchopekaji na uwakilishi wa kifonetiki	kategoria
/mkɔkɔteni/	/ɔmukɔkɔteni/	nomino
/mkate/	/ɔmukati/	nomino
/breki/	/ɛpuleki/	nomino
/msumenɔ/	/ɔmusumenɔ/	nomino
/mkɛka/	/ɔmukɛka/	nomino

Uchopekaji huu hutokea kwa sababu mfumo wa lugha ya Kinyore hauna mfumo wa silabi ya konsonanti pekee kwani ni lazima sauti ya konsonanti ifuatwe na irabu. Pili, ni rahisi kutamka konsonanti iliyo na irabu kuliko kutamka konsonanti pekee. Tatu, mfumo wa Kinyore unaruhusu mfumo wa kuunganisha sauti ya konsonanti na irabu. Uchopekaji wa irabu katika maneno mkopo hutekelezwa katika mazingira ya konsonanti mbili kufuatana. Irabu huweza kuchopekwa katikati mwa silabi mwambatano. Silabi pendwa huwa na muundo wa Konsonanti Irabu (KI), ili kupata muundo huu, maneno yaliyo na silabi mwambatano huweza kuchopekwa irabu katikati ili kupata muundo huo. Mfano ni neno msumeno lina silabi mwambatano ms ili kupata muundo wa KI, tunaongeza katikati irabu /u/ ili tuwe na silabi mu na neno liwe [ɔmusumeno]. Kwa kuunda silabi yenye muundo KI basi mawasiliano huwa yamerahisishwa.

3. 1. 1. 3 Ubadala

Ubadala ulidhihirika katika uchunguzi tuliofanya kwani kuna ubadala wa konsonanti na irabu. Konsonanti na irabu mbalimbali za Kiswahili zina vibadala vyake katika Kinyore. Maneno mkopo yasiyo na sauti za Kinyore yanapokopwa hizo sauti hupewa vibadala ambavyo ni sauti za Kinyore ili yakubalike katika Kinyore. Tumeangazia vibadala vya konsonanti na irabu.

i)Ubadala wa konsonanti

Kiswahili na Kinyore zinatofautiana pakubwa kwa upande wa konsonanti. Kuna utaratibu ambao maneno ya Kiswahili hupitia ili yakubalike katika Kinyore. Tofauti zilizoko baina ya konsonanti za Kiswahili na Kinyore ndizo zinazoleta mabadiliko katika maneno mkopo. Konsonanti zinazopatikana katika Kiswahili na hazipatikani katika Kinyore na ni /b/, /d/, /ʃ/, /g/, /v/, /z/, /h/, /ʃ/, /ɣ/, /ð/ na /θ/ (tazama 2.4). Kinyore kinapokumbana na hizi sauti geni huwa inazigeuza ili ziweze kutamkika kama za Kinyore.

i) /k/ > /k/, /s/ au /x/

Maneno ya Kiswahili yaliyo na sauti /k/ yanapokopwa na kuingizwa katika Kinyore mengine hubadilika kwa sababu sauti /k/ huweza kubadilika na kuwa /s/ au /x/. Baadhi ya maneno yaliyo na hiyo sauti hayapitii mabadiliko yoyote kwani /k/ ni sauti iliyo katika mfumo wa sauti wa Kinyore. /k/ na /s/ ni sauti zinazopatikana katika Kiswahili na Kinyore. /k/ ni kipasuo cha kaaka laini na /s/ ni kikwaruzo cha ufizi. /x/ ni sauti inayopatikana katika Kinyore si sauti ya Kiswahili. /x/ ni kikwaruzo cha kaaka laini. /k/ na /x/ ni sauti zilizo na uhusiano wa kifonetiki kwani zinatamkiwa mahali pamoja ambapo ni kaaka laini. /k/ ni kipasuo na /s/ na /x/ ni vikwaruzo kwa hivyo sauti /k/ huweza kudhoofika inapobadilika na kuwa /s/ na /x/.

19. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/k/	>	/s/
/kitanda/	>	/ɛsitanda/
/kikapu/	>	/ɛsikapo/

/kibeti/	>	/esipeti/
/kipimɔ/	>	/esipimɔ/
/kitjana/	>	/esitjanwa/
/kitfunji/	>	/esitfunjilo/
/kilimɔ/	>	/esilimɔ/
/kituo/	>	/esituo/

Sauti /k/ hubadilika na kuwa /s/ katika mazingira ya kufuatwa na irabu /i/.

/k/ → [s] / - /i/

Maneno mengi yanayoathiriwa wakati sauti /k/ inapobadilika na kuwa /x/ ni yale yanayopatikana katika ngeli ya 15 {ku-}.

20. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/k/	>	/x/
/kuɔta/	>	/ɔxwɔra/
/kuimba/	>	/ɔxwɛmba/
/kusɔma/	>	/ɔxusɔma/
/kuɔfa/	>	/ɔxusa:βa/
/kutjana/	>	/ɔxutjanula/

/kusuka/ > /ɔxusuka/

/kutɔra/ > /ɔxutɔra/

Sauti /k/ hubadilika na kuwa /x/ katika mazingira ya kufuatwa na vokali /u/.

/k/ → [x] / - /u/

Maneno mengine yaliyopitia haya mabadiliko yameorodheshwa hapa chini.

Kiswahili

Kinyore

/k/ > /x/

/kama/ > /xama/

/kata/ > /xalaka/

/kuza/ > /xusia/

/Pika/ > /tɛxa/

Kuna maneno ambayo hayapitii mabadiliko kwani sauti /k/ iko katika lugha zote mbili.

21. Mifano:

Kiswahili

Kinyore

/k/ > /k/

/mkɛbɛ/ > /ɔmukɛpɛ/

/kɛngɛɛ/ > /ɛkɛngɛɛ/

/kɔkɔtɔ/ > /ɛkɔkɔtɔ/

/kilo/	>	/ɛkilo/
/malaiika/	>	/malaiika/
/kamusi/	>	/ɛkamusi/
/karibu/	>	/kalipu/

ii)/J/ → /tʃ/

/tʃ/ ni sauti ya Kiswahili na Kinyore. Ili maneno mkopo yaliyo na sauti /J/ yaweze kukubalika katika Kinyore sauti /J/ ambayo si ya Kinyore huweza kubadilika na kuwa /tʃ/.

22. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/J/	>	/tʃ/
/Jumapili/	>	/tʃumapili/
/jembe/	>	/litʃembɛ/
/jambazi/	>	/litʃambasi/
/Januari/	>	/tʃanuari/
/jela/	>	/ɛtʃɛla/
/jeji/	>	/litʃɛsi/
/Jamhuri/	>	/tʃamu:ri/
/jasusi/	>	/tʃasusi/

Sauti /ʃ/ hubadilika na kuwa /tʃ/ katika mazingira ya kufuatwa na irabu.

/j/ → [tʃ] - /irabu/

iii) /v/ → /β/ au /f/

Kikwaruzo cha mdomo na meno /v/ huweza kubadilika na kuwa kikwaruzo cha mdomo na meno /f/ na kikwaruzo cha midomo /β/. Sauti /v/ na /f/ zina ukuruba mkuu wa kifonetiki kwani sauti zote ni za mdomo na meno na ni vikwaruzo. Sauti /v/ na /β/ zina ukuruba wa kiasi kwani sauti zote ni vikwaruzo. /v/ ni sauti inayopatikana katika Kiswahili lakini si sauti ya Kinyore. Maneno mkopo yaliyo na hii sauti huweza kupitia mabadiliko ili yakubalike katika Kinyore. Baadhi ya maneno yaliyo na sauti /v/ huweza kubadilika na kuwa /f/ ambayo ni sauti ya Kinyore na Kiswahili. Maneno mengine yaliyo na sauti /v/ huweza kupitia mabadiliko na sauti /v/ kubadilika na kuwa /β/ ambayo ni sauti ya Kinyore si sauti ya Kiswahili.

23. Mifano:

Kiswahili	>	Kinyore
/v/	>	/f
/mwavuli/	>	/limafuli/
/mlevi/	>	/ɔmulefi/

Maneno mkopo mengi yanayoathiriwa /v/ inapobadilika na kuwa /β/ ni yale hupatikana katika ngeli ya 8{vi}.


24. Mifano:

Kiswahili	>	Kinyore
/v/	>	/β/
/vikombe/	>	/εβikombε/

/vijiko/	>	/εβitjiko/
/vitumbua/	>	/εβitumbua/
/visima/	>	/εβisima/
/vitfaka/	>	/εβisaxa/
/viatu/	>	/εβilaro/

/v/ → [β] / - /i/

/v/ huweza hubadilika na kuwa /f/ na /β/ .




iv)/b/ → /p/

Kipasuo /b/ hubadilika na kuwa kipasuo /p/. Kinyore hakina sauti /b/ ndiposa maneno yaliyo na sauti /b/ yanapokopwa na kuingizwa katika Kinyore hiyo sauti hubadilika na kuwa /p/ ambayo ni ya Kinyore. /b/ ni sauti ya Kiswahili si sauti ya Kinyore, /p/ ni sauti ya lugha zote mbili. Hizi sauti zina ukuruba wa kifonetiki kwa sababu ni vipasuo vinavyotamkiwa midomoni. Tofauti iliyopo ni kwamba /b/ ni sauti ghuna na /p/ si sauti ghuna. Mabadiliko tulioeleza hutokea katika mazingira yoyote.

25. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/b/	>	/p/

/K**i**barua/ > /ε**s**i**p**arua/
 /**b**unduki/ > /ε**p**unduki/
 /**b**irika/ > /ε**p**irika/
 /**b**ima/ > /ε**p**ima/
 /**b**akuli/ > /ε**p**akuli/
 /**b**aruti/ > /ε**p**aruti/
 /**b**araka/ > /ε**p**araka/
 /**k**abila/ > /ε**k**apila/



v)/d/ > /t/

Hizi ni sauti zilizo na uhusiano wa karibu sana wa kifonetiki. Ni sauti zinazotamkiwa kwenye ufizi na ni vipasuo. Tofauti inayobainika ni kwamba /d/ ni sauti ghuna na /t/ si sauti ghuna. /d/ ni sauti ya Kiswahili lakini si ya Kinyore na /t/ ni sauti ya lugha zote mbili tulizoshughulikia. Maneno ya Kiswahili yaliyo na sauti /d/ yanapokopwa huwa yanapitia mabadiliko na hiyo sauti /d/ kubadilishwa na kuwa /t/.

26. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/d/	>	/t/
/doa/	>	/litɔa/

/dodo/ > /toto/
 /diriʃa/ > /litirisa/
 /dobi/ > /tɔpi/
 /dira/ > /ɛtila/
 /dakika/ > /ɛtakika/
 /madini/ > /amatini/
 /ʃahidi/ > /lisaiti/

/d/ → [t] - /v/

vi) /g/ > /k/

Sauti /g/ na /k/ ni vipasuo vya kaaka laini, kifonetiki vina ukuruba. Tofauti baina ya hizi sauti mbili ni kuwa /g/ ni sauti ghuna na /k/ si sauti ghuna. /k/ ni sauti ya lugha zote mbili. /g/ huweza kubadilishwa na kuwa /k/ ili ikubalike katika Kinyore.

27. Mifano:


Kiswahili		Kinyore
/g/	>	/k/
/gɔɔgɔɔ/	>	/kɔkɔkɔ/
/gazeti/	>	/likaseti/
/gari/	>	/likari/
/gundua/	>	/kundula/

/mzigɔ/ > /ɔmusikɔ/

/mhɔgɔ/ > /ɔmwɔkɔ/

/mtego/ > /ɔmutɛkɔ/

/ndege/ > /indɛkɛ/



vii) /gh/ > /k/

Kikwaruzo cha kaaka laini / gh / hubadilika na kuwa kipasuo cha kaaka laini /k/. Hizi sauti mbili zinahusiana kifonetiki kwa sababu zinatamkiwa mahali pamoja ambapo ni kaaka laini.

28. Mifano:

Kiswahili **Kinyore**

/gh / > /k/

/ ghorofa/ > /ɛkɔrɔfa/

/gharama/ > /ɛkarama/

/lughā/ > /ɛluka/

viii) /f/ > /s/

kikwaruzo cha kaaka gumu / f/ huweza kubadilika na kuwa kikwaruzo cha ufizi /s/. Vyote ni vikwaruzo vinavyotamkiwa mahali tofauti. / f/ ni sauti inayopatikana katika lugha ya Kiswahili lakini si sauti ya Kinyore. /s/ ni sauti inayopatikana katika lugha zote mbili tulizochunguza. Maneno mkopo yaliyo na sauti / f/ huweza kupitia mabadiliko ili hiyo sauti ibadilike na kuwa /s/ ndiposa iweze kukubalika katika mfumo wa sauti ya Kinyore.

29. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/f/	>	/s/
/filingi/	>	/ɛsilingi/
/fuka/	>	/lisuka/
/mfuma:/	>	/ɔmusuma/
/fetani/	>	/setani/
/fairi/	>	/lisairi/
/biafara/	>	/ɛβiasara/
/fuja:/	>	/sutfa:/
/feria/	>	/seria/
ix)/z/	>	/s/

Maneno ya Kiswahili yaliyo na kikwaruzo cha ufizi /z/ yanapokopwa sauti /z/ hubadilika na kuwa kikwaruzo cha ufizi /s/. Hizi sauti mbili zina ukuruba wa karibu sana wa kifonetiki kwa sababu zote ni vikwaruzo na hutamkiwa kwenye ufizi. Sauti /s/ ni sauti ya Kiswahili na Kinyore na sauti /z/ ni sauti ya Kiswahili na haiko katika mfumo wa sauti ya Kinyore na inapoingizwa katika Kinyore hubadilishwa ili kuchukua mfumo wa sauti ya Kinyore.

30. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/z/	>	/s/
/zaburi/	>	/ɛsapuli/
/mandazi/	>	/ama:ndasi/

/zumari/ > /isumari

x)/s/ > /s/

Maneno mengine ya Kiswahili yaliyo na sauti /s/ hayapitii mabadiliko yoyote kwa sababu /s/ ni sauti ya Kiswahili na Kinyore.

31. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/s/	>	/s/
/sindano/	>	/ɛsindani/
/soma/	>	/soma/
/simu/	>	/ɛsimu/
/makasi /	>	/likasi/
/siasa/	>	/ɛsiasa/
/kasisi/	>	/kasisi/
/hasara/	>	/asara/
/sukari/	>	/ɛsukari/
xi)/l/	>	/l/

Baadhi ya maneno yaliyo na kitambaza /l/ hubaki vivyo hivyo kwa sababu hii ni sauti ya Kiswahili na Kinyore.

32. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/l/	>	/l/

/lami/	>	/ɛlamu/
/kalamu/	>	/ɛkalamu/
/mlango/	>	/ɔmuliangɔ/
/lipa/	>	/lipa/
/gɔbli/	>	/ɛkɔbli /
/dalili/	>	/ɛtalili/
/lesɔ/	>	/ lilesɔ/

xii)/r/ > /r/ au /l/

Kimadende /r/ hubadilika na kuwa kitambaza /l/. Hizi sauti ni likwidi na zote zinatamkiwa kwenye ufizi, zina uhusiano wa kifonetiki wa karibu sana. Sauti /r/ hubaki hivyo kwa baadhi ya maneno yanayokopwa kwa sababu ni sauti ya Kiswahili na Kinyore.

33. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/r/	>	/l/
/suruali/	>	/ɛsiluali/
/dereva/	>	/ɔmundɛɛβa/
/risasi/	>	/lisasi/
/marupurupu/	>	/malupulupu/
/biringanya/	>	/ɛpilingana/
/bakora/	>	/ɛpakɔla/
/mkora/	>	/ɔmukɔla/

Kimadende /r/ kinachotamkiwa kwenye ufizi ni sauti ya Kinyore na Kiswahili. Maneno mkopo mengine hayabadiliki yanapokopwa kwa sababu /r/ ni sauti ya Kinyore.

34. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/r/	>	/r/
/rinda/	>	/lirinda/
/mrɛmbɔ/	>	/ɔmurɛmbɔ/
/karatasi/	>	/likaratasi/
/mrɛngɔ/	>	/ɔmurɛngɔ/
/starehe/	>	/ɛsitare:/
/uhuru/	>	/ɔbu:ru/
/ta:rifa/	>	/ɛta:rifa
/ɲara/	>	/ɲara/

ii)Ubadala wa irabu

Katika uchunguzi tuliofanya tuligundua kwamba ni irabu ya Kiswahili /i/ pekee iliyo na kabadala katika Kinyore na kabadala chake ni /ɛ/. /i/ ni vokali ya mbele na juu ambayo huweza kubadilika na kuwa irabu ya mbele na kati /ɛ/. Ukuruba mwingi wa kifonetiki ndio unaosababisha haya mabadiliko. Hizi sauti mbili hutamkwa midomo ikiwa imetanda na zote ni sauti ambazo hutamkiwa mbele. Hizi sauti mbili zina ujirani kwani /e/ ni sauti ya kati nayo /i/ ni sauti ya juu.

35. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/i/	>	/ɛ/
/tairi/	>	/litaɛli/

/imba/	>	/ɛmba/
/serikali/	>	/sɛlɛkali/
/karai/	>	/ɔlukaraɛ/

Katika mazingira ya kwanza /i/ imebadilika na kuwa /ɛ/ na katika mazingira mengine /i/ hubaki vivyo hivyo katika maneno mkopo.

36. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/i/	>	/i/
/kitabu/	>	/ɛsitapu/
/risiti/	>	/ɛrisiti/
/pipa/	>	/lipipa/
/jasusi/	>	/tʃasusi/
/ndimu/	>	/indimu/
/pilipili/	>	/ɛpilipili/
/kipini/	>	/ɛsipini/

3. 1. 1. 4 Kurefuka kwa irabu

Ukopaji wa maneno kutoka Kiswahili hadi Kinyore hufanya hayo maneno mkopo kuchukua miundo mbalimbali ya kifonetiki ya lugha pokezi ambayo ni Kinyore. Irabu za maneno mkopo ya Kiswahili huweza kubadilika zinapoingizwa katika Kinyore. Kinyore kina irabu tano ndefu na tano fupi. Kutokana na uchunguzi wetu ni irabu tu ndizo zinazobadilika na kuwa ndefu. Baadhi ya irabu za Kiswahili zinapoingizwa katika Kinyore huweza kubadilika na kuwa ndefu. Hili hutokea mara nyingi hasa wakati wa ukopaji wa vitenzi kama tulivyogundua kutokana na utafiti wetu.

37. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/andika/	>	/andi:ka/
/ruka/	>	/ru:ka/
/kanda/	>	/ka:nda/
/pima/	>	/pi:ma/
/lipa/	>	/li:pa/
/soma/	>	/so:ma/
/paka/	>	/ba:xa/
/lima/	>	/li:ma/
/Pangusa/	>	/paŋgu:sa/

3. 1. 1. 5 Silabi

Silabi wazi huishia kwa vokali na ndio muundo unaopendelewa sana na lugha nyingi za kibantu. Kinyore ni mojawapo ya lugha za kibantu kwa hivyo kimeweza kutumia huu muundo. Mabadiliko ya silabi yameweza kutokea katika maneno mkopo na mabadiliko haya yameweza kutokea kwa sababu ya tofauti baina ya maumbo ya silabi za Kiswahili na Kinyore. Lugha ya Kiswahili ina muundo wa silabi za konsonanti pekee muundo ambao haupo katika Kinyore. Maneno ya Kiswahili yaliyo na muundo wa konsonanti pekee yanapokopwa na kuingizwa katika Kinyore huweza kusilimishwa na kuchukua muundo wa konsonanti irabu ambao ni muundo unaopatikana katika Kinyore. Irabu huongezwa kwenye konsonanti na kufanya muundo wa konsonanti pekee wa Kiswahili kubadilika na kuchukua mojawapo ya maumbo ya silabi za Kinyore ambao ni konsonanti irabu.

Baada ya silabi /m/, vokali ya juu na nyuma /u/ huweza kuchopekwa na kulisababisha umbo la hapo awali la konsonanti pekee kubadilika na kuchukua umbo la silabi wazi ambalo huishia kwa vokali. Uchopekaji kati wa vokali huweza kutokea kila wakati Kinyore kinapokumbana na silabi

ya nasali /m/ na kuibadilisha kuwa na muundo wa konsonanti irabu. Maneno mengi ambayo hupitia haya mabadiliko hupatikana katika ngeli za 3 {mu} na 4 {mi}. Mifano iliyo hapa chini ilithibitisha uchopekaji kati wa irabu /u/ baada ya nasali /m/.

K > KI

38. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/m/	>	/mu/
mtunji	>	ɔmutunji
mkeka	>	ɔmukeka
mkebe	>	ɔmukepe
mswaki	>	ɔmuswaki
mswahili	>	ɔmuswaili
mchuzi	>	ɔmutfusi

Baada ya konsonanti /s/ irabu /i/ huchopekwa ili kupata muundo wa silabi pendwa.

39. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
/s/	>	/si/
askari	>	ɔmusikari
askofu	>	asikofu
stima	>	esitima

Sheria iliyotumika katika mabadiliko haya ni:

\$ K \$ > \$ KI \$

3.2 Hitimisho

Hii ni sura ambayo imeangazia mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea tunapokopa maneno kutoka Kiswahili na kuyaingiza katika Kinyore. Maneno yanapokopwa hupitia mabadiliko mbalimbali ili yaafiki muundo wa maneno ya Kinyore. Tumeangazia mabadiliko ya kifonimu ambapo tumeshughulikia mabadiliko yanayotokea kwenye konsonanti na irabu. Haya mabadiliko yameongozwa na kanuni za nadharia ya fonolojia leksika.

Ubadala hutokea kwa sababu mfumo wa sauti wa Kiswahili ni tofauti na mfumo wa sauti wa Kinyore. Baadhi ya maneno ya Kiswahili yana mfumo wa sauti ambao haupo katika Kinyore jambo ambalo linafanya hizi sauti kubadilishwa ili zichukue mfumo wa sauti wa Kinyore.

Muundo wa silabi za Kinyore na Kiswahili unatofautiana kwani Kiswahili kina muundo wa konsonanti pekee muundo ambao si wa silabi za Kinyore. Ili maneno yanayokopwa yaliyo na muundo huu yawe na muundo wa Kinyore uchopekaji wa irabu huweza kuyaleta haya mabadiliko. Irabu /u/ huchopekwa baada ya konsonanti ili kuleta muundo wa silabi za Kinyore ambao ni konsonanti irabu

SURA YA NNE

MIFANYIKO YA KIMOFOLOJIA

Utangulizi

Tumeshughulikia ngeli za Kinyore na Kiswahili . Tumeainisha hizo ngeli tukionyesha viambishi ambavyo vimetumika katika uainishaji huo. Otiende (2013) anasema kwamba kuainisha majina katika ngeli huwa sifa kuu ambayo hutambulisha lugha za kibantu. Otiende (2013) akimnukuu Iribemwangi (2010) anasema kuwa kuna njia ya nne ambayo hujumuisha hizo njia tatu tulizotaja.

Otiende (2013) anaeleza kuwa njia ya uainishaji wa ngeli kimofolojia ilitumika sana tangu jadi katika uchanganuzi wa lugha za Kibantu kama anavyoeleza Iribemwangi anapomtaja mwanaisimu Bleek (1869). Katika utafiti wetu tumetumia uainishaji wa kimofolojia kuainisha ngeli za Kiswahili na Kinyore. Mifanyiko ya kimofolojia tuliyoshughulikia kwenye hii sura ni uambishaji na unyambuaji.

4.1 Nomino ngeli za Kiswahili

Nomino kumi na nane zimetambulika katika uainishaji wa ngeli za Kiswahili nazo ni:

Ngeli 1 {mu-}

Nomino katika ngeli hii huwa na kiambishi ngeli {mu-}.

40. Mifano:

/ mu + alimu / [mwalimu]

/ mu + toto / [mtoto]

Ngeli 2 {wa-}

Ni ngeli inayowakilisha wingi wa ngeli ya kwanza. Huwa na kiambishi ngeli {wa-}

41. Mifano:

/wa + limu / [walimu]

/wa + tɔtɔ / [watɔtɔ]

Ngeli 3 {mu-}

Majina huchukua kiambishi ngeli {mu-}

42. Mifano:

/mu + undi / [mu:ndi]

/mu + ti / [mti]

Ngeli 4 {mi-}

Majina huchukua wingi wa ngeli ya tatu. Kiambishi ngeli kinachotumika hapa ni {mi-}.

43. Mifano:

/mi + ti / [miti]

/mi + undi / [miundi]

Ngeli 5 {ji / ϕ}

Mofu ya hii ngeli ni {ji-} na nyingine ni {ϕ}. Mofu kapa hupewa nomino ngeli zisizodhihirika kihalisia.

44. Mifano:

/ji + tʃɔ / [matʃɔ]

/ϕ + gɔti / [magɔti]

Ngeli 6 {ma-}

Hii ngeli huwakilisha wingi wa ngeli ya tano. Mofu ngeli hii hudhihirika hata kwa nomino ambazo huwa na mofu kapa.

45. Mifano:

/ ma + tʃɔ / [matʃɔ]

/ma + gɔti /] magoti]

Ngeli 7 {ki-}

Umbo la mofu ngeli hii huwa {ki-} na alomofu yake ni {tʃ-}.

46. Mifano:

/ tʃakula/ [tʃakula]

/ki + kɔmbɛ/ [kikɔmbɛ]

Ngeli 8 {vi-}

Ni wingi wa ngeli ya saba na huwakilishwa kwa kiambishi ngeli {vi-}.

47. Mifano:

/ vi + akula / [vyakula]

/vi + kɔmbɛ / [vikɔmbɛ]

Ngeli 9 {n /ɸ}

Maendelezo ya nomino katika ngeli hii huwa sawa katika umoja na wingi. Ngeli hii haina kiambishi maalum kinachoiwakilisha. Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa wataalam kama Carl Meinhorf wanasema pengine ngeli hii awali ilikuwa na kiambishi ngeli {n-} na kikadondoshwa kimapisi.

48. Mifano:

/ n + ʃulɛ / [ʃulɛ]

/ n + kalamu/ [kalamu]

Ngeli 10 {n/ ϕ}

Huwakilisha wingi wa ngeli ya 9. Tofauti baina ya ngeli 9 na 10 inadhihirika kifonolojia. Habwe na Karanja (2004) wanasema kwamba tofauti baina ya hizi ngeli mbili huonekana katika upatanisho wa kisarufi.

49. Mifano:

Shule imejengwa (9)

Shule zimejengwa (10)

Ngeli 11 { u-}

Majina katika ngeli hii huwa na kiambishi ngeli {u-} kilicho na alomofu { w-}.

50. Mifano:

/u + limi/ [ulimi]

/u + araka / [waraka]

/u + embε/ [wembε]

Ngeli 14 {u-}

Majina huchukua kiambishi ngeli ngeli { u-}.

51. Mifano:

/u + zuri/ [uzuri]

/u + tukufu/ [utukufu]

Ngeli 15 {ku-}

Kiambishi ngeli huwa { ku-} na ni ngeli ya vitenzi ambavyo hufanya kazi kama nomino.

52. Mifano:

/ku + tʃɛza/ [kutʃɛza]

ku + imba/ [kuimba]

Ngeli 16, 17, 18 { pa, ku, mu }

Hutumiwa kuonyesha hali mbalimbali za mahali. Ngeli ya 16 hurejelea mahali mahususi na huchukua kiambishi ngeli {pa-} kwa mfano: mahali hapa. Ngeli ya 17 huwa na kiambishi ngeli {ku-} na huonyesha mahali kwa jumla kwa mfano: mahali huku. Ngeli ya 18 huwa na kiambishi ngeli {mu-} na huonyesha mahali kuwa ndani kwa mfano: humu darasani.

4. 2 Nomino ngeli za Kinyore

Kulingana na utafiti wetu,tumegundua ya kwamba Kinyore kina nomino ngeli kama kilivyo Kiswahili. Tutaziainisha nomino ngeli za Kinyore kisha kuziwakilisha kwenye jedwali.

Ngeli 1{ɔmu-}

Ngeli hii huwakilishwa kwa mofu ngeli {ɔmu-} na alomofu yake ni {ɔmw-} na hutumiwa kuwakilisha hali ya umoja. Hali ya wastani ya majina ya binadamu huwakilishwa katika hii ngeli.

53. Mifano:

Nomino		Maana
/ɔmu + ndu/	[ɔmundu]	mtu
/ɔmu + lɔsi/	[ɔmulɔsi]	mchawi
/ɔmu + xaana/	[ɔmuxa:na]	msichana
/ɔmu + siani/	[ɔmusiani]	mvulana
/ɔmu + iβali/	[ɔmwiβali]	mwalimu

/ɔmu + ana/ [ɔmwana] motto

Ngeli 2 {aβa-}

Ngeli hii huonyesha maneno ya ngeli ya kwanza katika hali ya wingi. Kulingana na Otiende (2013) akimnukuu Guthrie (1947) anasema kwamba lugha za Kibantu huchukua {ba- } ya kihistoria kama kiambishi ngeli cha pili.

54. Mifano:

Nomino		Maana
/aβa + andu/	[aβa:ndu]	watu
/aβa + lɔsi/	[aβalɔsi]	wachawi
/aβa + xaana/	[aβaxa:na]	wasichana
/aβa + siani/	[aβasiani]	wavulana
/aβa + ana/	[aβa:na]	watoto

Ngeli 3 {ɔmu-}

Ngeli hii inawakilisha hali ya umoja wa nomino mbalimbali Otiende (2013) akimnukuu Palome (1967:97) anasema kwamba baadhi ya maneno yanayopatikana katika hii ngeli ni pamoja na majina ya vitu asili, sehemu za mwili na majina ya mimea. Kiambishi ngeli cha hii ngeli ni {ɔmu-} na {ɔmw-} ni alomofu yake.

55. Mifano:

Nomino		Maana
/ɔmu + xɔ ɲɛ/	[ɔmuxɔ ɲɛ]	miwa
/ɔmu + saala/	[ɔmusa:la]	mti
/ɔmu + rwe/	[ɔmurwe]	kichwa
/ɔmwɔ + kɔ	[ɔmwɔkɔ]	muhogo

/ɔmwɔ + si/ [ɔmwɔsi] moshi

Pia ngeli hii hushughulikia ukubwa wa nomino. Hali hii ya ukubwa huchukua kiambishi ngeli {ɔku-}

56. Mifano:

Nomino		Maana
/ɔku + ndu/	[ɔkundu]	jitu
/ɔku + rwe/	[ɔkurwe]	jichwa
/ɔku + limi/	[ɔkulimi]	limi
/ɔku + tuka/	[ɔkutuka]	jiduka
/ɔku + βusi/	[ɔkuβusi]	buzi

Ngeli 4 {ɛmi-}

Ngeli hii huonyesha wingi wa ngeli ya tatu na huwakilishwa kwa kiambishi ngeli {ɛmi-}.

57. Mifano:

Nomino		Maana
/ɛmi + xɔɲɛ/	[ɛmixɔɲɛ]	miwa
/ɛmi + saala/	[ɛmisa:la]	miti
/ɛmi + rwe/	[ɛmirwe]	vichwa
/ɛmi + ɔkɔ/	[ɛmiɔkɔ]	mihogo
/ɛmi + ndu/	[ɛmindu]	majitu
/ɛmi + limi/	[ɛmilimi]	malimi
/ɛmi + βusi/	[ɛmiβusi]	mabuzi

Ngeli 5 {eli- /li }

Kiambishi cha ngeli hii ni {eli-} na kina alomofu {li}. Badhi ya majina katika ngeli ni viungo vya mwili, majina ya wanyama na viumbe vya asili.

58. Mifano:

Nomino		Maana
/eli + nɔ/	[ɛlinɔ]	jino
/eli + ra/	[ɛlira]	jina
/ eli + kɔ/	[ɛlikɔ]	shimo
/li +tuma/	[lituma]	hindi
/li + xɔxɔ/	[lixɔxɔ]	ndege
/li + kunia/	[likunia]	gunia

Ngeli 6 [ama-}

Ngeli hii huonyesha wingi wa ngeli ya tano. Otiende (2013) anasema kuwa hii ngeli hujumuisha majina ya vitu viowevu kama vila mafuta. Ngeli hii huwa na kiambishi {ama-}.

59. Mifano:

Nomino		Maana
/ama + tʃi/	[amatʃi]	maji
/ama + fura/	[amafura]	mafuta
/ama + rasi/	[amarasi]	marashi

Ngeli 7{esi-}

Majina katika hii ngeli huchukua kiambishi ngeli {esi-} katika umoja.

60. Mifano:

Nomino		Maana
/ɛsi + tʃanwa/	[ɛsitʃanwa]	kichana
/ɛsi + pɛti/	[ɛsipɛti]	kibeti
/ɛsi + ɛjɔ/	[ɛsiɛjɔ]	ufagio
/ɛsi + lɛnjɛ/	[ɛsilɛnjɛ]	mguu
/ɛsi + fulia/	[ɛsifulia]	sufuria
/ɛsi + kɔmbɛ/	[ɛsikɔmbɛ]	kikombe

Ngeli 8 {ɛβi-}

Haya ni majina ya ngeli ya saba katika hali ya wingi na huchukua kiambishi ngeli {ɛbi-}.

61. Mifano:

Nomino		Maana
/ɛβi + tʃanwa/	[ɛβitʃanwa]	vichana
/ɛβi + pɛti/	[ɛβipɛti]	vibeti
/ɛβi + ɛjɔ/	[ɛβiɛjɔ]	fagio
/ɛβi + lɛnjɛ/	[ɛβilɛnjɛ]	miguu
/ɛβi + fulia/	[ɛβifulia]	sufuria
/ɛβi + kɔmbɛ/	[ɛβikɔmbɛ]	vikombe

Ngeli 9 {iN-}

Ngeli hii inajumuisha majina ya wanyama na nomino za kawaida. Ngeli hii ina kiambishi ngeli {iN-}.

62. Mifano:

Nomino		Maana
/iN + busi/	[imbusi]	mbuzi
/iN+ ηgɔxɔ/	[iηgɔxɔ]	kuku
/iN+bwa/	[imbwa]	mbwa
/iN+gɔmbe/	[iηɔmbe]	ng'ombe

Alomofu za {iN-} ni {in-}, {im-}, {iη} na {iɲ}

Ngeli 10

Hii ngeli huwakilisha wingi wa nomino za ngeli ya tisa. Nomino za ngeli ya tisa hazibadiliki katika hali ya wingi kwa hivyo nomino za ngeli ya tisa ndizo za ngeli ya kumi.

Ngeli 11 {ɔlu-}

Kiambishi ngeli cha nomino za hii ngeli ni {ɔlu-}.

63. Mifano:

Nomino		Maana
/ɔlu + karaɛ/	[ɔlukaraɛ]	karai
/ɔlu + tɛlu/	[ɔlutɛlu]	uteo
/ɔlu + mɔ/	[ɔlumɔ]	wembe
/ɔlu + xailɔ/	[ɔluxailɔ]	ya kukata nyasi
/ɔlu + paŋga/	[ɔlupaŋga]	upanga

Ngeli 12 {axa-}

Hii ngeli haipatikani katika Kiswahili sanifu lakini inatumika katika Kinyore kudunisha nomino. Kiambishi ngeli cha nomino za hii ngeli ni {axa-}.

64. Mifano:

Nomino		Maana
/axa + ana/	[axa:na]	kitoto
/axa + βwa/	[axaβwa]	kijibwa

Wingi wa hizi nomino hupatikana katika ngeli ya 7.

65. Mifano:

Nomino		Maana
/εβi + ana/	[εβiana]	vitoto
/εβi + βwa/	[εβiβwa]	vijibwa

Ngeli 14{ɔβu-}

Majina katika ngeli hii yana kiambishi ngeli {obu-}.

66. Mifano:

Nomino		Maana
/ɔβu + lwaε/	[ɔβulwaε]	ugonjwa
/ɔβu + lai/	[ɔβulai]	uzuri
/ɔβu + sɔmi/	[ɔβusɔmi]	usomi
/ɔβu + kɔra/	[ɔβukɔra]	ukora

/ɔβutaxa/ [ɔβutaxa] umaskini

Nomino nyingi katika hii ngeli hazina hali ya wingi.

Ngeli 15 {ɔxu-}

Hii ngeli hutumika kwa vitenzi vinavyofanya kazi kama nomino na ina kiambisi ngeli {oxu-}.

67. Mifano:

Nomino		Maana
/ɔxu + tɛxa/	[ɔxutɛxa]	kupika
/ɔxu + lima/	[ɔxulima]	kulima
/ɔxu + sina /	[ɔxusina]	kucheza
/ɔxu + andika/	[ɔxuandika]	kuandika
/ɔxu + kanda/	[ɔxuka:nda]	kukanda

Ngeli ya 17 mahali {xu -}

Hii ngeli hutumika kuonyesha mahali kwa ujumla na huwa na kiambishi ngeli {xu-}

68. Mifano:

Nomino		Maana
/xu + njila/	[xunjila]	barabarani
/xu + sirɔ/	[xusirɔ]	sokoni
/xu + ndɛβ ɛ/	[xundɛ βɛ]	kitini
/xu + sikulu/	[xusikulu]	shuleni

Ngeli ya 18 {mu-}

Hii ngeli hutumika kuonyesha undani wa mahali na kiambishi ngeli chake ni {mu-}na ina alomofu {mw-}

69. Mifano:

Nomino		Maana
/mu + kanisa/	[mukanisa]	kanisani
/mw + ipafu/	[mwipafu]	bafuni
/mw +ituka/	[mwituka]	dukani

Kielelezo 4.1 Jedwali la ngeli za Kinyore

Nambari	Ngeli	Mifano ya nomino	Maana
1	{omu-}	omundu, omusomi, omuxae	Mtu, msomi, mke
	{omw-}	omwitfuxulu, omwana, omwami	Mjukuu, mtoto, mfalme
2	{aβa-}	aβandu, aβasomi, aβaxae aβe:xo, aβa:na, aβa:mi	Watu, wasomi, wake Wajukuu, watoto, wafalme
	{omu-}	omusa:la, omukoe, omutata	Mti, kamba, mfuko
3	{omw-}	omwoko, omwoyo	Mhogo, moyo
	{oku-}	okubusi, okukati, okuβwa	Buzi, jikate, jibwa
4	{emi-}	emisa:la, emitata, emioko, emioyo	Miti, mifuko, mihogo, mioyo
5	{eli-}	eliandu, elino, eliolu	Taka, jino, pua
	{li-}	lisafu, likomia, liru	Jani, ndizi, jani la ndizi
6	{ama-}	Amandu, amasafu, amolu, amakomia, amaru	Taka, majani, pua, ndizi, majani ya ndizi

7	{esi-}	esikombe, esitifikō, esilarō	Kikombe, kijiko, kiatu
8	{εβi-}	εβikombe, εβitifikō, εβilarō	Vikombe, vijiko, viatu
9	{iN}	imbusi, iḡombe, imbwa	Mbuzi, ng'ombe, mbwa
10	{iN}	imbusi, iḡombe, imbwa	Mbuzi, ḡombe, mbwa
11	{olu-}	olusimbi, olukaraε, olutelu	Taji, karai, uteo
12	{axa-}	axa:na, axakalamu, axandu	Kitoto, kijikalamu, kijitu
14	{obu-}	oburembō, obulwae, obubi	Urembo, ugonjwa, ubaya
15	{oxu-}	oxusuma, oxusisa, oxusuxania	Kutafuta, kusugua, kugeuza
17	{xu-}	xusirō, xusiku:lu	Sokoni, shuleni
18	{mu-}	Mukanisa, mutfō:	Kanisani, msalani

4.3 Mifanyiko ya kimofolojia

Tumechunguza mifanyiko ya kimofolojia inayokumba maneno yanapokopwa kutoka Kiswahili na kuingizwa katika Kinyore. Tumeangazia uambishaji wa maneno mkopo kwa sababu kuna baadhi ya maneno ambayo yanapokopwa na kuingizwa katika Kinyore hupata viambishi ili yakubalike katika Kinyore. Maneno mengine hunyambuliwa ili yakubalike katika Kinyore. Nadharia ya fonolojia leksika imetuongoza katika michakato tuliyoshughulikia. Kanuni ya mpangilio wa viambishi imetumika katika kazi hii kwani imetusaidia kuonyesha jinsi maneno mkopo yanavyopokea viambishi mbalimbali yanapoingizwa katika Kinyore. Kanuni ya kufuta mabano imetusaidia hapa kwa sababu baada ya kuunda umbo la ndani mabano hufutwa ili umbo la nje liweze kupatikana. Viambishi vya ndani huwekwa kwenye shina baadaye viambishi vya nje vikaongezwa na kupata umbo la neno mkopo.

4.3.1 Uambishi

Mara nyingi maneno yanapokopwa viambishi mbalimbali huongezwa kwenye neno mkopo ili liweze kukubalika katika Kinyore. Kiambishi awali /e/ huongezwa kwenye baadhi ya nomino zinazopatikana katika ngeli ya 7 {ki} na 9 {n/ϕ}.

70. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
kiboko	>	εiboko
kikombe	>	εikombe
kibuju	>	εibuju
sufuria	>	εifulia
meza	>	εmesa
sejenge	>	εijenge
kahawa	>	εkawa
uma	>	εuma
pamba	>	εpamba

Kiambishi awali /i/ huongezwa kwenye maneno mkopo ya Kiswahili ili kuafiki muundo wa maneno ya Kinyore. Maneno mengi yanayoathirika hapa yanapatikana katika ngeli ya 9 {n/ϕ}.

71. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
ndoo	>	indo
mbuzi	>	imbusi

mbwa	>	imbwa
ɲumba	>	ɪɲumba
ɲama	>	ɪɲama
ɲgamia	>	ɪɲgamia
ndururu	>	indururu

Maneno mkopo mengine huchukua kiambishi awali /ɔ/ .

72. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
msusi	>	ɔmusuki
mkulima	>	ɔmulimi
mwiko	>	ɔmwixɔ
mɟipi	>	ɔmusipi
mfereji	>	ɔmufeletɟi
msɔmaji	>	ɔmusɔmi
mpifi	>	ɔmutexi

Maneno mengine huchukua silabi ya awali /li/ ili kuafiki muundo wa maneno ya Kinyore.

73. Mifano:

Kiswahili		Kinyore
yai	>	liyai
koti	>	likoti
dɛɛ	>	liteɛ

kanisa	>	likanisa
tiṅgatiṅga	>	litiṅgatiṅga
embe	>	liembe
fenesi	>	lifenesi

Katika uambishi wa irabu tuliojadili hapo awali, irabu hizi ni silabi kamili mwanzoni mwa neno. Irabu zinapoongezwa kwenye neno huongeza idadi ya silabi na kubadilisha umbo la neno la lugha changizi ambayo ni Kiswahili na kulifanya lichukue umbo la neno la lugha pokezi ambayo ni Kinyore. Silabi /li/ huchopekwa mbele ya maneno mkopo na muundo wa maneno hubadilika na kuchukua muundo wa maneno ya Kinyore.

4.3.2 Unyambuaji

Unyambuaji ni utaratibu katika lugha wa kuongezea viambishi kwenye mzizi wa maneno ili kuunda maneno mapya (Habwe na Karanja 2004). Mfano wa unyambuaji ni kuunda nomino kutokana na vitenzi kwa kutumia viambishi. Unominishaji ni hali ya kuunda nomino kutoka kwa kategoria nyingine za maneno. Nomino zinaweza kuundwa kutoka kwa vitenzi kwa kuongeza mofimu {- i} kwenye mzizi.

74. Mifano:

Neno mkopo	Unominishaji	Nomino	Tafsiri
baxa	{ ɔmu + bax + i }	ɔmubaxi	wa kupaka
soma	{ ɔmu + sɔm + i }	ɔmusɔmi	msɔmaji
kanda	{ ɔmu + kand + i }	ɔmukandi	anayekanda
suka	{ ɔmu + suk + i }	ɔmusuki	msusi
pima	{ ɔmu + pim + i }	ɔmupimi	mpimaji
emba	{ ɔmu + emb + i }	ɔmuembi	mwimbaji

Nomino nyingine zinaweza kuundwa kwa kuongeza mofimu {-o} kwenye mzizi wa vitenzi.

75. Mifano:

Neno mkopo	Unominishaji	Nomino	Tafsiri
soma	{ ama + sɔm + ɔ }	amasɔmɔ	masɔmɔ
pima	{ esi + pim + ɔ }	esipimɔ	kipimɔ
emba	{ ɔlu + emb + ɔ }	ɔluembɔ	wimbo
lima	{ esi + lim + ɔ }	esilimɔ	kilimo

Mofu {oxu-} huweza kuongezwa kwenye maneno mkopo ili kuunda nomino kutokana na vitenzi. Huu unominishaji huathiri maneno yanayopatikana katika ngeli ya 15 (oxu-)

76. Mifano:

Neno mkopo	Unominishaji	Nomino	Tafsiri
emba	{ ɔxu + emb + a }	ɔxuemba	kuimba
lima	{ ɔxu + lim + a }	ɔxulima	kulima
pima	{ ɔxu + pim + a }	ɔxupima	kupima
baxa	{ ɔxu + bax + a }	ɔxubaxa	kupaka
kanda	{ ɔxu + kand + a }	ɔxukanda	kukanda

4 . 4 Hitimisho

Tumeshughulikia nomino ngeli za Kiswahili sanifu na za Kinyore. Tumeangazia viambishi ngeli ambavyo huwekwa kwa nomino katika kila ngeli katika hali ya umoja na wingi. Tumbaini kwamba kuna nomino ambazo katika hali ya umoja na wingi hubaki vivyo hivyo hazibadiliki. Hizi nomino zinapatikana katika lugha zote mbili tulizofanyia utafiti. Mifanyiko ya kimofolojia tuliyoshughulikia katika hii sura ni uambishaji na unyambuaji.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

Utangulizi

Sura hii imetoa muhtasari wa uchunguzi wetu na mapendekezo yanayotokana na uchunguzi huu kama tulivyojadili katika sura ya pili, tatu na nne. Katika uchanganuzi wetu tumetumia mihimili ya nadharia ya fonolojia leksika.

5.1 Muhtasari

Lugha tulizofanyia utafiti ni Kiswahili na Kinyore na zote ni lugha za kibantu. Tumeangalia fonimu za hizi lugha mbili tukiangazia irabu na konsonanti. Kuna mwingiliano wa fonimu za hizi lugha mbili. Kiswahili kina sauti ghuna na si ghuna lakini mfumo wa Kinyore unapendelea sauti si ghuna. Maneno yaliyo na sauti zisizo katika mfumo wa sauti ya Kinyore yanapokopwa hubadilika ili yakubalike katika Kinyore.

Mifumo ya sauti ya hizi lugha mbili inafanana na kutofautiana kwa sababu kuna sauti zinazopatikana katika lugha zote, kuna zenye zinapatikana katika Kiswahili lakini haziko katika Kinyore na kuna za Kinyore ambazo ziko katika Kiswahili.

Kiswahili na Kinyore zina miundo ya silabi wazi na muundo ambao lugha zote mbili zinapendelea ni wa KI na lugha zote mbili zina miundo ya KI na I. Hili jambo ndilo linaloleta tofauti kuu baina ya hizi lugha mbili. Maneno mkopo yasiyo na sauti na silabi za Kiswahili hupitia mabadiliko ili yakubalike katika mfumo wa sauti wa Kinyore. Muundo wa konsonanti pekee wa Kiswahili unapoingia katika Kinyore hubadilika na kuwa KI kwa sababu Kinyore kina huu muundo na hakina muundo wa silabi wa K.

Tumeangazia mifanyiko ya kifonojia inayokumba sauti za irabu na konsonanti ambayo maneno mkopo hupitia ili yakubalike katika Kinyore. Baadhi ya mifanyiko ni uchopekaji, udondoshaji, ubadala, uambishaji na unyambuaji. Maneno mengine hayapitii mabadiliko yoyote kwani hubaki tu jinsi yanavyokopwa. Uambishaji hutokea wakati ambapo neno lililokopwa huongezwa viambishi. Umbo la nje hutokana na kuongezea viambishi umbo la ndani na viambishi vyenyewe

huwa katika viwango. Kiwango cha kwanza ni viambishi vinavyokaribia mzizi na vya nje ni vile vinavyopatikana kwenye muundo wa nje.

5.2 Matokeo ya utafiti

Madhumuni yetu yalituelekeza katika huu uchunguzi na baada ya kushughulikia fonimu za lugha zote mbili; Kiswahili na Kinyore, tuligundua ya kwamba Kiswahili kina idadi kubwa ya fonimu kuliko Kinyore, Kiswahili kina konsonanti ishirini na tano na Kinyore kina kumi na sita. Konsonanti zinazopatikana katika lugha zote mbili ni vipasuo /p/, /t/, /k/, zinazopatikana katika Kiswahili na haziko katika Kinyore ni /b/, /d/, /g/ na / ʃ /. Vikwaruzo vya Kiswahili ni /h/,/s/,/z/,/v/,/f/,/ ʃ/,/ ɣ/, /θ/, /ð/na vya Kinyore ni /β/,/f/,/s/,/x/. Vikwaruzo vya Kiswahili na Kinyore ni /f/,/s/ na vya Kiswahili ambavyo haviko katika Kinyore ni /h/,/z/,/v/,/ ʃ/,/ ɣ/, /θ/, /ð/. Lugha zote mbili zina kipasuo- kwaruzo /tʃ/. Lugha zote mbili zina idadi sawa ya nasali nazo ni /m/, /n/,/p/, /ŋ/. Viyeyusho vinavyopatikana katika lugha zote mbili ni /w/ na /j/.

Utafiti wetu umethibitisha kuwepo kwa maneno mkopo ya Kiswahili katika Kinyore. Mifanyiko mbalimbali imeonyesha jinsi maneno yanavyopitia mabadiliko ili yakubalike katika Kinyore. Sauti za Kiswahili hupitia mabadiliko mbalimbali ili zikubalike katika Kinyore. Konsonanti za Kiswahili ambazo si sauti za Kinyore hupitia mabadiliko ili zikubalike katika Kinyore. Baadhi ya konsonanti za Kiswahili ambazo hubadilika ni /b/, /g/, / ʃ /, /d/, / ɣ /, /z/, /v/, / ʃ/. Hizi sauti zina vibadala vyake katika Kinyore, zinapokopwa zinabadilika na kuwa za Kinyore.

Irabu za Kinyore ni kumi, tano fupi na tano ndefu / ε, ε:, i, i:, a, a:, ɔ, ɔ:, u, u:/ na za Kiswahili ni tano/ ε, i, a, ɔ, u/. Maneno mkopo huchukua miundo mbalimbali ya kifonetiki ya lugha pokezi.. Baadhi ya irabu za maneno mkopo huimarika kwa mfano neno la Kiswahili andika hubadilika na kuwa *andi:ka*. Maneno yaliyo na sauti ambazo zinapatikana katika mifumo yote miwili ya lugha hayapitii mabadiliko yoyote yanapoingia katika Kinyore.

Udondoshaji na uchopekaji umedhihirisha mabadiliko ya fonimu za irabu na konsonanti na kubainisha mazingira ya kifonetiki. Maneno ya Kiswahili yaliyo na muundo wa silabi wa K hupitia uchopekaji ili yapate muundo wa silabi ulio katika mfumo wa sauti wa Kinyore. Utafiti huu umedhihirisha uchopekaji wa irabu mbili /i/ na /u/ kwenye maneno mkopo. Uchopekaji na udondoshaji ni mifanyiko ambayo inafanya maneno yakubalike.

Mifanyiko ya kimofolojia imedhihirisha uambishi mwanzo wa irabu kwenye maneno ya Kinyore. Uambishaji huu umedhihirika katika maneno mkopo kwa sababu viambishi mbalimbali vimeongezwa kwa maneno mkopo ili yakubalike katika Kinyore. Baadhi ya viambishi hivi ni / ε -, /i-, /ɔ -, /li-.

Ngeli mbalimbali zimeshughulikiwa katika lugha zote mbili kwani tumeainisha ngeli za Kiswahili na za Kinyore. Tumeainisha ngeli za lugha zote mbili katika makundi kumi na nane japo kuna baadhi ya ngeli ambazo zilikosa nomino kwa mfano Kiswahili hakina nomino katika ngeli ya ngeli ya 12 {ka-} na 13 {ki-}. Nomino zimeainishwa kwa kutumia viambishi ngeli kwa hivyo kila ngeli ina kiambishi ngeli chake kinachoitambulisha. Ngeli hizi huathiriwa wakati wa ukopaji kwa sababu ili neno likubalike katika Kinyore huchukua viambishi ngeli vya Kinyore.

Nadharia ya fonolojia leksika ilitusaidia kuweka wazi mifanyiko tuliyoshughulikia. Ilitusaidia kutambua maumbo ya ndani na jinsi neno linavyoundwa kutokana na hili umbo la ndani. Kanuni za ngazi leksia, kimzunguko, mpangilio wa viambishi na kufuta mabano ndizo zilizotuongoza katika uchanganuzi wetu. Zilitusaidia kuweka wazi mifanyiko ya kifonolojia na kimofolojia inayoyakumba maneno yanayokopwa. Pia zilitusaidia kujua jinsi umbo la nje linavyotokana na umbo la ndani na kuelezea kuwa umbo la ndani ndilo linalosababisha kuwepo kwa umbo nje.

Maneno mkopo yamesaidia Kinyore kukua kwa mfano badala ya Kinyore kuwa na neno moja la mwalimu lina kisawe chake katika Kinyore [ɔmwiβali]. Ukopaji umetumika kufidia ukosefu wa msamiati wa dhana geni katika Kinyore kwa mfano [tʃɛɾɛhani] ni neno lililokopwa kwa nia hiyo na lilipoingizwa katika Kinyore likawa [ɛsitʃɛɾɛani]. Hapakuwa na msamiati mwingine wa kutajia hicho kifaa ndiposa neno hilo likakopwa. Matokeo yetu yanaonyesha kwamba vigezo tofauti hutawaliwa na kanuni bayana.

5.3 Mapendekezo

Maneno mkopo yalichunguzwa na ndharia ya FL. Mifanyiko ya kifonolojia na kimofolojia ilihusu mabadiliko yaliyotokea kwenye fonimu na silabi. Kinyore kina toni. Huu utafiti wetu haukushughulikia toni. Pana haja ya utafiti zaidi kufanywa ili kubaini mabadiliko ya toni yanayotokea kwenye maneno mkopo.

Huu ukopaji umeshughulikia mifanyiko inayotokea kwenye maneno mkopo katika viwango vya kifonolojia na kimofolojia. Pana haja ya utafiti kufanywa utakaoshughulikia ukopaji katika viwango vya kisintaksia na kisemantiki.

Utafiti huu ulichunguza maneno mkopo kutoka Kiswahili hadi Kinyore. Pana haja ya tafiti kufanywa kuhusu maneno mkopo kutoka lugha nyingine kwa sababu hapo awali tulitaja kwamba Kinyore kilikopa maneno kutoka lugha nyingine kama lugha nyingine za Kibantu na Kiingereza.

Nchini Kenya wizara ya elimu imekuwa ikisisitiza wanafunzi wafunzwe miaka ya kwanza shuleni kwa kutumia lugha ya kwanza. Uchunguzi wetu unatoa mapendekezo ya kwamba vitabu vya kufunzia Kinyore vihakikiwe ili viwe na maneno mkopo kwa sababu Kinyore sasa kina maneno mkopo mengi sana.

Wanahabari na watangazaji wa idhaa za Kinyore wanaweza kutumia hii data ya maneno mkopo wanapokumbana na msamiati geni katika harakati zao za utangazaji. Matokeo ya utafiti huu yanaweza kutumiwa na wakalimani na watafsiri wanaotafsiri Kiswahili hadi Kinyore.

6.0 MAREJELEO

- Angogo, R. (1983) *Unity in Diversity. A Linguistic Survey of the Abaluyia of Western Kenya. EAAC*
- Akidah, M. A (2012) *A Lexical Phonology Study of Modern Standard Arabic (MSA). Unpublished PhD Thesis. University of Nairobi.*
- Bakari, M. (1982) *The Morphophonology of the Kenyan Swahili Dialects. Tasnifu ya Uzamifu, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.*
- Chomsky, N na Halle, (1968) *The Sound Pattern of English. New York: Harper & Publishers*
- Habwe na Karanja (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili, Nairobi: Phoenix Publishers.*
- Habwe, Matei na Nyonje (2010) *Darubini ya Isimujamii, Nairobi:Phoenix Publishers.*
- Itabete, P. (1974) *Language Standardisation in Western Kenya*
- International Phonetic Association (2018) www.langsci.ucl.ac.uk/IPA Chart (c) 2018.pdf.
- Iribemwangi na Mukhwana (2011) *Isimujamii, Nairobi: Printpak.*
- Katamba, F. (1989) *An Introduction toPhonology. London: Longman*
- Kiparsky ,P. (1982) *From Cyclic to Lexical Phonology, Dordrecht:Foris Publication.*
- Malanda, M. S (2005) *A Synchronic Study of the Major Phonological Processes of the Luyore and Lutachoni Dialects of Luyia Consonantal Systems.*

- Unpublished Masters Thesis. University of Nairobi.
- Massamba, D. P. (1999) *Sarufi Miundo ya Kiswahili*. Dar – es Salaam: TUKI
- Massamba, D. P. B (2011) *Maendeleo Katika Nadharia ya Fonolojia*, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Mathooko, M. (2007) *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njuguna Books. Educational Publishers
- Mgullu, R. S (1999) *Mtalaa wa Isimu*, Longhorn Publishers.
- Mulwa, N. M. (2014) *Fonolojia ya Nomino mkopo za Kikamba Kutoka Kiswahili. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa*. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mwaliwa, C. H. (2000) *Ulinganishi wa Mofofonolojia ya Kiswahili na Kidawida: University of Nairobi*. Nairobi.
- Mwaliwa, C. H. (2014) *An Analysis of the Syllable Structure of Standard Kiswahili Loanwords from Modern Standard Arabic: Unpublished PhD Thesis: University of Nairobi*.
- Mwihaki, A. N (1998) *Loanword Nativisation: A Generative view of the Phonologic Adaptation of Gikuyu Loanwords*, Doctoral Thesis, Kenyatta University.
- Ochilo, G. O. (2018) *The Effects of Dholuo on Lunyore: A Case of Lexical Borrowing*. Unpublished Thesis: University of Nairobi.

- Otiende, M. A (2013) Athari za Kimofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili Sanifu kama Lugha ya Kwanza. Tasnifu ya uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Shidiavai, M. S (2015) Aphonological Analysis of Lwidakho Loanwords from Kiswahili And English, Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Were, G. (1967) *Western Kenya Historical Texts: Abaluyia, Teso and Elgon Kalenjin*. EAACB

VIAMBATANISHI

Maneno mkopo kutoka Kiswahili hadi Kinyore

Data

Mahojiano ya redio

Kiswahili	Kinyore	Alama za kifoneti
1. Pesa	amapesa	/amapesa/
2. Saa	esaa	/esaa/
3. Simu	esimu	/esimu/
4. Leso	lilesa	/lilesa/
5. Kipindi	esipindi	/esipindi/
6. Meza	emesa	/emesa/
7. Madini	amatini	/amatini/
8. Watalii	abatilii	/abatilii/
9. Vyama	ebiama	/ebiama/
10. Siasa	esiasa	/esiasa/
11. Stima	esitima	/esitima/
12. Daraja	etalacha	/etalatʃa/
13. Kitabu	esitapu	/esitapu/

14. Kijiko	esichiko	/ɛsitʃikɔ/
15. Kabati	ekabati	/ɛkaβati/
16. Shati	lisaati	/lisa:ti/
17. Cherehani	echereani	/ɛtʃɛɾɛani/
18. Bei	epei	/ɛpei/
19. Gunia	likunia	/likunia/
20. Kitunguu	esitunguyu	/ɛsitunguju/
21. Nazi	linasi	/linasi/
22. Hema	liema	/liɛma/
23. Mpira	omupira	/ɔmupira/
24. Sahani	esaani	/ɛsa:ni/
25. Mbolea	imbolela	/imbɔlələ/
26. Sukari	esukari	/ɛsukari/
27. Mkate	omukati	/ɔmukati/
28. Msumeno	omusumeno	/ɔmusumɛnɔ/
29. Kamusi	ekamusi	/ɛkamusi/
30. Mkebe	omukepe	/ɔmukɛpɛ/
31. Kengele	ekengele	/ɛkɛŋgɛlɛ/
32. Kupima	okhupima	/ɔxupi:ma/
33. Kusoma	okhusoma	/ɔxuso:ma/
34. Pika	okhutekha	/ɔxutɛ:xa

35. Mwavuli	limafuli	/limafuli/
36. Kichana	esichanua	/ɛsitʃanua/
37. Nyanya	enyanya	/ɛnɔnɔ/
38. Jeshi	lichesi	/litʃɛsi/
39. Godoro	omukotolo	/ɔmukɔtɔlɔ/
40. Barua	eparua	/ɛparua/
41. Duka	lituka	/lituka/
42. Shoka	esoka	/ɛsɔkɔ/
43. Kifungo	esifungo	/ɛsifungɔ/
44. Ghasia	ekasia	/ɛkasia/
45. Raha	eraa	/ɛra:/
46. Harambee	arambee	/arambɛ:/
47. Haleluya	aleluya	/alaluja/
48. Mkeka	omukeka	/ɔmukɛkɔ/
49. Kibeti	esipeti	/ɛsipeti/
50. Kichungi	esichungilo	/ɛsitʃungilɔ/
51. Kituo	esituo	/ɛsituo/
52. Pipa	lipipa	/lipipa/
53. Jasusi	chasusi	/tʃasusi/
54. Kikombe	esikombe	/ɛsikɔmbɛ/
55. Chupa	echupa	/ɛtʃupa/

56. Ghorofa	ekorofa	/ɛkɔrɔfa/
57. Kalamu	ekalamu	/ɛkalamu/
58. Mwalimu	mwalimu	/mwalimu/
59. Ubao	olupao	/ɔlupao/
60. Serikali	eselekali	/ɛsɛlekali/
61. Dirisha	litolisa	/litolisa/
62. Rinda	lirinda	/lirinda/
63. Sindano	esindani	/ɛsindani/
64. Gari	likari	/likari/
65. Dakika	etakika	/ɛtakika/
66. Starehe	esitaree	/ɛsitarɛ:/
67. Bakora	epakora	/ɛpakɔra/
68. Sheria	eseria	/ɛseria/
69. Mandazi	amandasi	/amandasi/
70. Ndururu	indururu	/indururu/
71. Biashara	ebiasara	/ɛβasara/
72. Mshumaa	omusuma	/ɔmusuma/
73. Ndimu	indimu	/indimu/
74. Pilipili	epilipili	/ɛpilipili/
75. Doa	litoa	/litoa/
76. Hasara	asara	/asara/

77. mwiko	omwikho	/ɔmwixɔ/
78. anua	anula	/anula/
79. steni	esitendi	/ɛsitendi/
80. Tairi	litaeli	/litaeli/
81. Maslahi	amasilai	/amasilai/
82. Vipodozi	ebipotosi	/ɛβipɔtɔsi/
83. Embe	liembe	/liɛmbɛ/
84. Pamba	ɛpamba	/ɛpamba/
86. Kibuyu	esibuyu	/ɛsiβuju/
87. Mchuzi	omuchusi	/ɔmutʃsi/
88. Mswaki	omuswaki	/ɔmuswaki/
89. Kipini	esipini	/ɛsipini/
90. Ng'ara	ng'ara	/ŋara/

BIBLIA NA MAKTABA

91. Zaburi	esapuri	/ɛsapuri/
92. Kanisa	likanisa	/likanisa/
93. Baraka	ɛparaka	/ɛparaka/
94. Askofu	asikofu	/asikɔfu/
95. Kasisi	kasisi	/kasisi/
96. Shetani	setani	/setani/
97. Uhuru	obuuru	/ɔβu:ru/

98. Taarifa	etaarifa	/eta:rifa/
99. Karatasi	likaratasi	/likaratasi/
100. Lami	elamu	/elamu/
101. Risasi	lisasi	/lisasi/
102. Gharama	ekarama	/ekarama/
103. Lugha	eluka	/eluka/
104. Shuka	lisuka	/lisuka/
105. Shairi	lisairi	/lisairi/
106. Kanda	kaanda	/ka:nda/
107. Karae	olukarae	/ɔlukarae/
108. Lipa	liipa	/li:pa/
109. Lima	liima	/li:ma/
110. Mstari	omusitari	/ɔmusitari/
111. Askari	omusikari	/ɔmusikari/
112. Mswahili	omuswaili	/ɔmuswaili/
113. Sengenge	esing'enge	/esiŋeŋge/
114. Kahawa	ekawa	/ekawa/
115. Shahidi	lisaiti	/lisaiti/
116. Bunduki	epunduki	/epunduki/
117. Makasi	amakasi	/amakasi/
118. Birika	lipilika	/lipilika/

119. Sufuria	esifuria	/ɛsifuria/
120. Uma	euma	/ɛuma/
121. Ndo	indoo	/indoː/
122. Mshipi	omusipi	/ɔmusipi/
123. Mfereji	omufelechi	/ɔmufɛletʃi/
124. Debe	litepe	/litepe/
125. Tingatinga	litingatinga	/litingatinga/
126. Kibarua	esiparua	/ɛsiparua/
127. Bakuli	epakuli	/ɛpakuli/
128. Dalili	etalili	/etalili/
129. Dereva	omundeleba	/ɔmundeleβa/
130. Ngamia	ingamia	/iŋgamia/
131. Msomaji	omusomi	/ɔmusomi/
132. Mkokoteni	omukokoteni	/ɔmukɔkɔtɛni/
133. Shtaki	okhusitaka	/ɔxusitaka/
134. Jamhuri	chamuuri	/tʃamuːri/
135. Jumapili	chumapili	/tʃumapili/
136. Jumamosi	chumamosi	/tʃumamɔsi/
137. Jumatatu	chumatatu	/tʃumatatu/
138. Kokoto	ekokoto	/ɛkɔkɔtɔ/
139. Kuchora	okhuchora	/ɔxutʃɔra/

140. Jambazi	lichambasi	/litʃambasi/
141. Hoho	eoo	/ɛo:/
142. Bendera	ependera	/ɛpɛndɛra/
143. Firimbi	efilimbi	/ɛfilimbi/
144. Meli	emeli	/ɛmeli/
145. Njugu	injuku	/injuku/
146. Pasi	epasi	/ɛpasi/
147. Pingu	epingu	/ɛpingu/
148. Sabuni	esabuni	/ɛsaβuni/
149. Sadaka	esataka	/ɛsataka/
150. Nyundo	inyundo	/ijnundɔ/
151. Gololi	ekololi	/ɛkɔlɔli/
152. Ruhusa	erusa	/ɛrusa/
153. Kipimo	esipimo	/ɛsipimɔ/
154. Kuosha	okhusaaba	/ɔxusa:βa/
155. Kibeti	esipeti	/ɛsipɛti/
156. Kamua	khama	/xama/
157. Kata	khalaka	/xalaka/
158. Kuza	khusia	/xusia/
159. Karibu	kalipu	/kalipu/
160. Dira	etila	/ɛtila/

161. Gorogoro	omukolokolo	/ɔmukɔləkɔlə/
162. Mzigo	omusiko	/ɔmusikɔ/
163. Ghafila	kafula	/kafula/
164. Shujaa	suchaa	/sutʃaː/
165. Zumari	isumali	/isumali/
166. Wakili	wakili	/wakili/
167. Kinyozi	esinyosi	/ɛsɪnɔsi/
168. Suruali	esiluali	/ɛsiluali/
169. Marupurupu	malupulupu	/malupulupu/
170. Mrengo	omurengo	/ɔmureŋgɔ/
171. Jangili	lichangili	/litʃaŋgɪli/
172. Vitumbua	ebitumbua	/ɛβitumbua/
173. Baruti	epaluti	/ɛpaluti/
174. Dodo	toto	/tɔtɔ/
175. Dobi	topi	/tɔpi/
176. Koti	likoti	/likɔti/
177. Chungwa	lichungwa	/litʃuŋgwa/
178. Fenesi	lifenesi	/lifɛnesi/
179. Bakora	epakora	/ɛpakɔra/
180. Mrembo	omurembo	/ɔmurembɔ/

